Haliuzwi
APRIL 20, 2026
/islamicftz
Dhul-Qadah 3 1447
# IMAAN
ISSN 5618 - NO. 580
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Nauli Zapanda, wadau wa usafiri washinikiza Serikali kupunguza tozo za mafuta




# Mauzo Sukuk yaonesha dalili njema sokoni




Hafla ya uzinduzi wa Sukuk iliyowakutanisha Benki ya KCB, wawakilishi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), pamoja na wadau wa sekta hiyo

**Soko la vipodozi vya Halal kufikia dola Bilioni 162 ifikapo 2034**

## Maboresha afya yamtambulisha Rais Samia Kimataifa



**Viongozi Uganda waonya kushuka viwango vya mafunzo ya Qur'an**

## Licha ya taharuki Ghuba, taasisi zasema Hijja iko salama



## UNICEF yailaumu Israel kwa mauaji ya wasambazaji misaada

SARA ZUBERI

# Mapato Sukuk yaonesha dalili njema siku za awali za mauzo

**CIFCA, Kituo cha Uzingatiaji na Ushauri wa Huduma za Kifedha za Kiislamu (Centre for Islamic Finance, Compliance and Advice), ambacho kimekuwa mstari wa mbele katika uratibu, utetezi na uwezeshaji wa miamala ya fedha inayotii Shari'ah, kiliwakilishwa na viongozi wake wakuu wakiwemo Mwenyekiti Aref Nahdi na Katibu Mkuu, Salum Lupande.**

Mkuu wa Kitengo cha Benki ya Kiislamu katika KCB Sahl Banking, Amour Muro, amesema mwitikio wa wawekezaji kwa Mapato Sukuk iliyozinduliwa wiki umekuwa wa kuridhisha, huku akieleza kuwa dalili za awali zinaonesha uwezekano mkubwa wa kufikia au hata kuzidi lengo la ukusanyaji wa fedha.

Akizungumza katika mahojiano na Gazeti Imaan, Muro alisema tangu kufunguliwa kwa dirisha la uwekezaji Aprili 15, 2026, Watanzania wa kada mbalimbali wameanza kujitokeza kwa wingi, wakivutiwa na bidhaa hiyo ya kifedha inayozingatia misingi ya Shari'ah.

"Mwitikio ni mzuri kwa kweli. Tunaona watu wanapiga simu, wanakuja na wanawekeza... tunadunduliza na tuna uhakika tutafikia malengo yetu," alisema Muro.

Hafla ya uzinduzi wa Sukuk hiyo, wiki iliyopita, iliwakutanisha viongozi waandamizi wa Benki ya KCB, wawakilishi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), pamoja na wadau wa sekta hiyo, wakiwemo wateja wa benki hiyo.

CIFCA, Kituo cha Uzingatiaji na Ushauri wa Huduma za Kifedha za Kiislamu (Centre for Islamic Finance, Compliance and Advice), ambacho kimekuwa mstari wa mbele katika uratibu, utetezi na uwezeshaji wa miamala ya fedha inayotii Shari'ah, kiliwakilishwa na viongozi wake wakuu wakiwemo Mwenyekiti Aref Nahdi na Katibu Mkuu, Salum Lupande.

Mwenyekiti Nahdi, akizungumza na gazeti hili baadae, alisema taasisi yake wanaridhishwa na kufurahishwa na hatua za maendeleo zinazopigwa katika huduma za kifedha za Kiislamu husussan katika uwekezaji wa halal na hasahasa eneo la Sukuk.

"Tunaona juhudi zetu za utetezi, uenezi, hamasa zinalipa sasa, na hili linatupa faraja sana," alisema Mwenyekiti Nahdi.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi, Mapato Sukuk ni uwekezaji wa muda wa miaka mitatu, ukianza mwaka 2026 na kukamilika rasmi Mei 28, 2029. Ndani ya kipindi hicho, wawekezaji wanatarajiwa kupata faida ya takribani asilimia 11 kwa mwaka, inayolipwa kila baada ya miezi mitatu na hatimaye, kama kawaida, kurejeshewa mitaji yao mwishoni.

Lengo la Mapato Sukuk ni kukusanya takribani shilingi bilioni 10. Hata hivyo, muundo wa uwekezaji huu unaruhusu ongezeko la hadi bilioni 20 iwapo kutakuwa na mwitikio mkubwa wa wawekezaji.

Muro alisema dalili za awali zinaonesha uwezekano huo, kutokana na ushiriki wa wawekezaji binafsi, vikundi na taasisi.

Dirisha la uwekezaji limefunguliwa Aprili 15, 2026 na linatarajiwa kufungwa Mei 14, 2026. Baada ya hapo, faida zitakuwa zinalipwa katika vipindi vya Agosti, Novemba, Februari na Mei kila mwaka hadi mwisho wa uwekezaji.

Aidha, Sukuk hii itaanza kuuzwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kuanzia Juni 3, 2026, hatua itakayowezesha uwekezaji huu kuuzwa na kununuliwa katika soko la upili.

## Fursa kwa wote — si Waislamu pekee

Muro alisisitiza kuwa bidhaa hii haijalenga Waislamu pekee bali kila mtu anayevutiwa na uwekezaji unaozingatia maadili. Alieleza kuwa hata wasiokuwa Waislamu wameonesha kuvutiwa nayo kwa sababu fedha zao hazitaelekezwa katika sekta kama kamari, pombe au tumbaku.

"Ni uwekezaji salama na wa kimaadili, ndiyo maana watu wengi wanaupokea vizuri," alisema.

Kwa kuongeza, kiwango cha chini cha uwekezaji cha shilingi 500,000 kimewekwa ili kurahisisha ushiriki wa wananchi wengi zaidi, hatua inayolenga kupanua ujumuishaji wa kifedha nchini.

Kwa mtazamo wa soko, Muro anaonya kuwa wawekezaji wa awali wana nafasi ya kunufaika zaidi kabla ya Sukuk kuingia kwenye DSE, ambapo bei na upatikanaji vitaanza kuathiriwa na nguvu za soko.

"Baada ya kuorodheshwa, mtu atalazimika kununua kutoka kwa aliyewekeza awali. Na kwa kuwa wengi watashikilia uwekezaji wao, wanunuzi wanaweza kuwa wengi kuliko wauzaji," alieleza.

## Historia na uaminifu: KCB yajenga rekodi

## KCB si mgeni katika soko hili.

Mwaka 2022, Benki ya KCB Tanzania iliandika historia kwa kuzindua Fursa Sukuk, hati fungani ya kwanza ya Kiislamu nchini na katika Ukanda wa Afrika Mashariki, hatua iliyothibitisha dhamira yetu ya kukuza ujumuishaji wa kifedha kwa kutoa fursa za uwekezaji kwa watu wa imani zote.

Muro anakumbusha kuwa Suku yao hiyo ya kwanza ilikamilika kwa mafanikio makubwa mwaka 2025, ambapo wawekezaji wote walilipwa mtaji wao pamoja na gawio bila matatizo yoyote.

"Hakuna mtu aliyeachwa. Hii imejenga imani kubwa kwa wawekezaji wetu," alisema. Rekodi hii inaonekana kuwa moja ya sababu zinazochochea matumaini ya mafanikio ya Mapato Sukuk ya sasa.

## Enzi mpya ya uwekezaji wa kimaadili?

Kwa ujumla, mwitikio wa awali wa Mapato Sukuk unaashiria muendelezo wa mwelekeo mpya katika soko la fedha Tanzania — kuelekea bidhaa zinazochanganya faida ya kiuchumi na misingi ya kimaadili.

Kwa ufafanuzi, Sukuk ni chombo cha uwekezaji kinachofanana kwa muundo na hati fungani, lakini hutegemea shughuli halisi za kibiashara badala ya riba.

DHUL QADAH 3,

ذُو القِعدة




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha Maalum



## Hafla ya uzinduzi wa Sukuk iliyowakutanisha Benki ya KCB, wawakilishi kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), pamoja na wadau wa sekta hiyo







DHUL QADAH 3,

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU




# Licha ya taharuki Ghuba, taasisi zasema Hijja 1447 iko salama

Wakati hali ya taharuki iliyosababishwa na mvutano wa kijeshi kati ya Iran, Israel na washirika wake ikianza kutulia kufuatia kusimamishwa kwa mapigano, taasisi za kusafirisha mahujaji nchini zimewataka Waislamu kuendelea na maandalizi ya Hijja bila hofu, zikisisitiza kuwa hakuna athari kubwa zilizobaki zinazoweza kuvuruga ibada hiyo mwaka huu.

Katika wiki zilizopita, hofu ilitanda miongoni mwa Waislamu duniani kufuatia ongezeko la mashambulizi ya kijeshi katika eneo la Mashariki ya Kati.

Hali hii ilizua wasiwasi juu ya usalama wa Saudi Arabia—mahali panapofanyika ibada ya Hijja—pamoja na uwezekano wa kuvurugika kwa safari za ndege kutokana na kufungwa au kubadilishwa kwa njia za anga.

Wachambuzi wa masuala ya usalama walionya kuwa iwapo mgogoro huo ungeendelea, ungeweza kuathiri moja kwa moja ratiba za safari za mahujaji, kuchelewesha au hata kufuta baadhi ya safari, hasa kwa nchi zinazotegemea njia za anga zinazopita katika ukanda huo.

Kulikuwepo pia hofu ya kupanuka kwa mashambulizi hadi nchi za Ghuba, ikiwamo Saudi Arabia, jambo ambalo lingekuwa na athari kubwa kwa ibada ya Hijja.

Ikumbukwe kuwa Mwishoni mwa Machi na mwanzoni mwa Aprili 2026, Iran ilianzisha mashambulizi kadhaa ya makombora na ndege zisizo na rubani (drones) yakilenga Saudi Arabia, na ncgi nyingine za Ghuba ambapo ilishambulia miundombinu muhimu ya kijeshi na nishati.

Hata hivyo, kufuatia hatua za kidiplomasia na kupungua kwa mashambulizi ya moja kwa moja, hali ya usalama imeanza kurejea katika viwango vinavyoruhusu shughuli za kawaida kuendelea, ikiwemo safari za kimataifa za anga.

Katika mahojiano na gazeti la Imaan, viongozi wa taasisi mbalimbali za Hijja nchini wamesema maandalizi yanaendelea kama kawaida na hakuna taarifa rasmi zinazoashiria hatari yoyote kwa mahujaji wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Idara ya Hijja na Umra katika Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), Alhaj Haidar Kambwili, alisema kuwa hadi sasa taratibu zote muhimu zimekamilika, ikiwemo malipo ya mahema, hoteli, tiketi za ndege na chanjo, huku usajili wa mahujaji ukiwa tayari umefungwa.

Alisema Bakwata inatarajia kusafirisha mahujaji 100 mwaka huu, ambao wataondoka mwanzoni mwa mwezi Mei kupitia Shirika la Ndege la Oman Air.

Kwa upande wake, kiongozi kutoka taasisi ya Peace Travel & Tours, Sheikh Haruna Kapama maarufu Abu Hafswa, alisema taasisi yao imesajili mahujaji 60 ambao tayari wamekamilisha vipimo vya afya katika Hospitali ya Shifaa jijini Dar es Salaam, na wote wameonekana kuwa na afya njema.

Aliongeza kuwa hadi sasa hawajakutana na changamoto yoyote inayohusiana na mgogoro huo, akitolea mfano safari za Umra zilizofanyika hivi karibuni ambapo mahujaji wote walirejea salama nchini.

"Hatuna taarifa yoyote ya kutia wasiwasi. Maandalizi yote yamekamilika, tunasubiri siku ya safari tu," alisema Kapama.

Aidha, aliwataka mahujaji watarajiwa kupuuza taarifa zisizo rasmi zinazosambazwa mitandaoni ambazo zimekuwa zikizua taharuki, na badala yake wategemee maelekezo kutoka katika taasisi rasmi za Hijja.

Naye Katibu wa taasisi ya Al-Husna Hajj Trust, Ahmed Kizigo, alisema wao pia hawajakumbana na changamoto yoyote, huku wakitarajia kusafirisha mahujaji 60 watakaoondoka nchini Mei 17 mwaka huu baada ya kukamilika kwa taratibu zote muhimu ikiwemo visa, tiketi na maandalizi ya afya.

Sambamba na kukamilika kwa maandalizi ya kiutawala na usafiri, taasisi nyingi sasa zimeingia katika hatua ya mwisho ya maandalizi—kuwapa mafunzo mahujaji watarajiwa.

Mafunzo hayo yanalenga kuwaandaa kitaaluma kuhusu taratibu na ibada za Hijja, kuwajengea utayari wa kisaikolojia kukabiliana na mazingira ya ibada yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, pamoja na kuwapa mwongozo wa kimwili ili waweze kustahimili changamoto za kiafya na kimazingira wakati wa ibada hiyo.

Hatua hii inaonekana kuwa sehemu muhimu ya maandalizi ya kisasa ya Hijja, ikilenga kuhakikisha mahujaji si tu wanafika salama, bali pia wanatekeleza ibada zao kwa ufanisi na utulivu wa akili.

Kwa ujumla, licha ya taharuki iliyotokana na mvutano wa kijeshi katika Mashariki ya Kati, taasisi za Hijja nchini zinaeleza kuwa hali ya sasa ni tulivu na inaruhusu maandalizi ya ibada hiyo kuendelea kama ilivyopangwa.

Mwelekeo huu unaashiria kwamba, angalau kwa sasa, hofu ya kuvurugika kwa Hijja kutokana na mgogoro wa kikanda imepungua, huku mamlaka na wadau wa usafiri wa anga wakiendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama ili kuhakikisha safari za mahujaji zinafanyika kwa utulivu na usalama.

NA MWANDISHI WETU

# Jitihada kuboresha huduma za afya zamtambulisha Rais Samia Kimataifa

## WFNS Yamtunuku tuzo maalumu ya ubinadamu

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali imepiga hatua kubwa katika kuimarisha huduma za upasuaji wa ubongo nchini, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuboresha huduma za kibingwa na kuongeza upatikanaji wa matibabu ya kuokoa maisha.

Akifungua mkutano wa pili wa Kimataifa wa Shirikisho la Jumuiya za Upasuaji wa Ubongo Duniani (WFNS), jana, Rais Samia alisema Tanzania imeongeza idadi ya hospitali zinazotoa huduma za upasuaji wa ubongo kutoka mbili zilizokuwapo miaka mitano iliyopita hadi saba kwa sasa.

Alisema hatua hiyo ni matokeo ya uwekezaji endelevu katika miundombinu ya afya na huduma za kibingwa, ukilenga kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma hizo ndani ya nchi bila kulazimika kusafiri nje.

Katika hotuba yake, Rais Samia pia alibainisha ongezeko kubwa la wataalamu wa afya nchini, akisema idadi ya wataalamu wa tiba katika nyanja mbalimbali imepanda kutoka 138 mwaka 2020 hadi 1,518 mwaka 2026 ni mageuzi makubwa kwenye sekta ya afya nchini.

Kwa upande wa wataalamu wa upasuaji wa ubongo (neurosurgeons), alisema wameongezeka kutoka 12 hadi 37, ambapo saba kati yao ni wanawake ishara ya ongezeko la ushiriki wa wanawake katika fani za kitabibu zilizokuwa zikichukuliwa kuwa ngumu na za kiufundi zaidi.

Aidha, alieleza kuwa Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya afya kupitia mpango wa bima ya afya kwa wote, ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, pamoja na matumizi ya mifumo ya afya ya kidijitali ili kuongeza ufanisi na uendelevu wa huduma.

Rais Samia alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya afya duniani katika kukabiliana na changamoto zinazochangiwa na mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya vipaumbele vya kimataifa, pamoja na maendeleo ya kisiasa na kiuchumi. Katika hatua nyingine, Rais alitunukiwa tuzo maalumu ya ubinadamu ya upasuaji wa ubongo kutokana na mchango wake katika kuimarisha huduma za afya na hususan upasuaji wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu nchini.

Akikabidhi tuzo hiyo, Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Tanzania, Dk Othman Kiloloma, alisema uongozi wa Rais Samia umeleta mageuzi makubwa katika sekta ya afya, hasa katika kuokoa maisha ya wagonjwa wa magonjwa ya ubongo na uti wa mgongo. Alibainisha kuwa Tanzania imeongeza uwezo wa kukabiliana na magonjwa hatarishi ya ubongo na uti wa mgongo kupitia uwekezaji wa rasilimali watu, miundombinu na teknolojia.

Kwa upande wake, Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa alisema kuwa Serikali inaendelea kuwekeza katika vituo vya kisasa vya tiba kama Kituo cha Sayansi ya Mishipa ya Fahamu cha Mloganzila, upanuzi wa huduma katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), pamoja na kuanzishwa kwa teknolojia za kisasa za uchunguzi na vituo vya urekebishaji.

> **"Mafanikio haya yanaonesha dhamira yetu ya kuimarisha uwezo wa kitaifa na kupanua upatikanaji wa huduma za kibingwa kwa wananchi wote."** Rais Samia




**Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo maalumu ya ubinadamu (Humanitarian award) ya upasuaji wa ubongo aliyokabidhiwa na Shirikisho la Jumuiya za Upasuaji wa Ubongo Duniani (WFNS) kutokana na mchango wake katika kuimarisha huduma za afya.**

NA MWANDISHI WETU
DAR ES SALAAM

# Nauli Zapanda, wadau washinikiza Serikali kupunguza tozo za mafuta

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), imetangaza ongezeko katika nauli mpya zitakazotumika kuanzia Mei mosi mwaka huu.

Aprili 8, 2026 Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Dk Habibu Suluo wakati wa kikao kilichoandaliwa na taasisi hiyo kupokea maoni ya wadau wa usafirishaji, alieleza kuwa, upokeaji wa maoni utaendelea hadi Aprili 21 ili kutoa fursa zaidi kwa wasiopata nafasi kuwasilisha mapendekezo yao kwa mfumo wa barua pepe lakini Aprili 17, Mwenyekiti wa Bodi ya Latra, Ahmed Ame alitangaza nauli mpya.

Kwa mujibu wa tangazo lililopo katika Gazeti la Serikali la Aprili 17, 2026, taarifa ya kawaida namba 5996 Ame alieleza kuwa, Latra imefanya mapitio ya viwango vya nauli za vyombo vya usafiri ardhini na kwamba, nauli mpya za mabasi ya masafa marefu, mabasi ya mijini (daladala), teksi mtandao na pikipiki mtandao zitakuwa kama zilivyoainishwa.

Kutokana na mabadiliko hayo kwa kila nauli ya daladala imeongezeka Sh100 nauli ya chini itakuwa Sh700 badala ya Sh600 iliyokuwapo (kwa safari chini ya kilometa 10) na kwa safari yenye urefu kati ya kilometa 36 na 40 nauli itakuwa Sh1500, badala ya Sh1400.

Ame alirejea kuwa mapatio hayo yamezingatia kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 kimetoa mamlaka kwa Latra kupanga na kufanya mapitio ya viwango na tozo za huduma za usafiri ardhini.

"Umma unataarifiwa zaidi kuwa, nauli hizi zitaanza kutumika siku kumi na nne tangu tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii na Latra itafuatilia utekelezaji wa viwango vya nauli vilivyowekwa katika taarifa hii," inaeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha ongezeko la bei limeenda sambamba na ongezeko la wigo la nauli ya kianzio kwa taksi mtandao, bajaji mtandao na bodaboda ambapo kiwango cha chini cha teksi kitakuwa Sh6,000, bajaji Sh3,000 na bodaboda Sh1,500.

Kwa sehemu kubwa msukumo wa kuongeza bei ulitokana na ongezeko la bei ya mafuta duniani kufuatia kuvurugika kwa uzalishaji na usambazaji wa nishati hiyo muhimu tangu kuibuka kwa vita kati ya Israel, Marekani dhidi ya Iran.


Kufuatia tangazo hilo wadau wa usafirishaji wakiwamo wamiliki wa mabasi na daladala walisema wamepokea kwa mikono miwili hatua ya nyongeza kidogo ya nauli ingawa si kubwa lakini wanashukuru Mungu.

"Tunashukuru kwa hiki kidogo maana usiposhukuru kwa kidogo huwezi kupata kikubwa maana gharama za uendeshaji zimepanda hivi sasa," alisema Sabri Mabrouk ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Daladala (Darcoboa). Kauli hiyo ya Mabrouk iliungwa mkono na Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Priscus John aliyesema wanaishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio chao.

"Nauli imepanda si kwa sababu tunatafuta faida bali kupunguza gharama za uendeshaji, walichokifanya Latra ni kukidhi gharama zetu za mafuta katika shughuli zetu za kila siku. Hata hivyo, tunashukuru kwa hicho hicho kidogo, sio mbaya maana tunapambana sana haikuwa kazi rahisi kama watu wanavyodhani," alisema John.

Hata hivyo John Essau mtumiaji wa daladala alisema ongezeko hilo lilipaswa kusubiri kwa muda ili kupata mwelekeo halisi wa bei ya mafuta kwani hata bei ikishuka baadaye haoni nauli ikishushwa na imekuwa hivyo mara zote.

"Kilichosababisha kupanda kwa bei ya mafuta kinaweza kuisha muda wowote kwani ni mgogoro unaohusisha masilahi ya watu wengi duniani, Latra ingejipa muda kidogo ili kuona mwelekeo halisi maana walivyopandisha hivi hata mafuta yakishuka hawatoshusha tena," alisema Essau.



# Tanzania ya tatu Afrika kwa mazingira bora ya uwekezaji



Tanzania imeendelea kuimarisha nafasi yake kama kivutio cha kimataifa cha uwekezaji kutoka nje, kwa mujibu wa ripoti ya World Investment Report 2025.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo Aprili 16, 2026 alipokuwa akikazia baadhi ya mambo muhimu baada ya kuwasilisha makadirio ya bajeti ya shilingi bilioni 144.85 kwa wizara yake kwa mwaka wa fedha 2026/27.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Tanzania imeendelea kuimarisha utendaji wake katika mtiririko wa uwekezaji wa sekta binafsi ambapo uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za Marekani bilioni 1.72 mwaka 2024, ikilinganishwa na dola bilioni 1.34 mwaka 2023 sawa na ukuaji wa asilimia 28.3.

Katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ilishika nafasi ya tatu kwa kuvutia uwekezaji kutoka nje, nyuma ya Ethiopia iliyovutia takribani dola bilioni 3.98 na Uganda yenye dola bilioni 3.31.

Tanzania ilizipita Kenya iliyovutia takribani dola bilioni 1.50 na Rwanda iliyovutia takribani dola milioni 819.

Kwa ujumla, takwimu hizo zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye ukuaji wa haraka wa uwekezaji barani Afrika, ikishika nafasi ya 11 kwa ukubwa wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI).

## Bunge Tanzania laridhia Bunge la Kiarabu kupewa hadhi ya mwangalizi

**Bunge la Tanzania limeunga mkono azimio la kulipa Bunge la Kiarabu hadhi ya mwangalizi ndani ya Mtandao wa Mabunge ya Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM–PN).**

**Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daniel Sillo, alitoa kauli hiyo Aprili 15, 2026 alipohutubia Mkutano wa Tano wa Mabunge ya NAM–PN uliofanyika katika Hoteli ya Hilton Istanbul Bomonti, jijini Istanbul, Uturuki.**

**Katika mkutano huo, Sillo alimwakilisha Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu, na aliambatana na Mbunge Elibariki Kingu.**

**Akizungumza katika mkutano huo, Sillo alisema azimio hilo limezingatia maombi rasmi yaliyowasilishwa na Bunge la Kiarabu la kutaka kupatiwa hadhi ya mwangalizi katika mtandao huo.**

**"Bunge la Tanzania linaunga mkono azimio la kulipa Bunge la Kiarabu hadhi ya mwangalizi ndani ya mfumo wa NAM–PN," alisema Sillo.**

**Hadhi hiyo ikitolewa, Bunge la Kiarabu litashiriki katika vikao na shughuli za NAM–PN kama mwangalizi, hatua inayotarajiwa kuimarisha ushirikiano wa mabunge na kukuza malengo ya pamoja ya nchi wanachama wa Harakati ya Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote.**

**Sillo alisisitiza kuwa uamuzi huo uliopitishwa na mabunge wanachama, ikiwemo Tanzania, unaakisi dhamira ya kujenga madaraja ya ushirikiano kati ya Tanzania na nchi za Kiarabu zilizo chini ya Bunge la Kiarabu, pamoja na kuimarisha diplomasia ya kibunge katika ngazi ya kimataifa kama sehemu ya kuimarisha ujenzi wa taasisi na kuongeza ufanisi wa utendaji wa NAM–PN.**

## Benki ya Dunia yaipa Tanzania dola mil 550 kusaidia elimu, kaya masikini

**Benki ya Dunia kupitia Bodi yake ya Wakurugenzi imeiidhinishia Tanzania dola za Marekani milioni 550, sawa na zaidi ya shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili ya kimkakati katika sekta za elimu na kusaidia kaya masikini.**

**Uamuzi huo umetangazwa na Makamu wa Rais wa benki hiyo Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Dkt. Ndiame Diop, alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, pembezoni mwa Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika makao makuu ya taasisi hizo jijini Washington, D.C, Marekani.**

**Kati ya fedha hizo, dola za Marekani milioni 300 zitatumika kusaidia programu ya elimu ya kuongeza ujuzi, hususan kwa vijana, na dola milioni 250 zitatumika kusaidia kaya masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).**

## Ajira mpya 45,000 zanukia

**Serikali imepanga kuajiri watumishi wapya 45,000 katika mwaka wa fedha 2026/27 katika taasisi za umma, pamoja na kutoa vibali vya ajira mbadala kwa watumishi 7,124 wa kada mbalimbali.**

**Hata hivyo, Kamati ya Bunge imependekeza kufanyika kwa maboresho ya mfumo wa ajira kwa kuruhusu waombaji wenye sifa na vyeti vya ngazi mbalimbali kushiriki katika usaili wa nafasi za kazi zinazotangazwa, bila kuwekewa vikwazo visivyo vya lazima vinavyohusiana na kiwango cha elimu.**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete alisema hayo Aprili 17, 2026 wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2026/27, ambapo aliomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.6.**

**Alisema katika bajeti hiyo, Serikali pia itafanya uhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma katika taasisi 425, pamoja na mishahara katika taasisi 127 zinazotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi (e–Watumishi).**




UKHTI FATIMA SS

# Soko la vipodozi vya Halal kufikia dola Bilioni 162 ifikapo 2034

Soko la kimataifa la vipodozi vya halal linatarajiwa kufikia dola bilioni 162.44 ifikapo mwaka 2034, likikua kwa kasi ya asilimia 13.2 kila mwaka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa salama na zenye maadili.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa soko, thamani ya sekta hiyo imeongezeka kutoka dola bilioni 47.01 mwaka 2025, ikionyesha mwelekeo mpya wa watumiaji kuelekea bidhaa zisizo na viambato vilivyokatazwa kama pombe na baadhi ya bidhaa za wanyama.

Wataalamu wanasema ukuaji huo hauchochewi na Waislamu pekee bali pia watumiaji wa kawaida wanaotafuta bidhaa safi, rafiki kwa mazingira na zisizo na ukatili kwa wanyama.

Sekta hiyo pia inanufaika na ukuaji wa biashara mtandaoni, ambapo majukwaa ya kidijitali na mitandao ya kijamii yanaongeza upatikanaji wa bidhaa za halal duniani.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa Asia na Mashariki ya Kati vinaongoza soko hilo, huku Ulaya na Amerika Kaskazini zikijitokeza kama masoko mapya yenye fursa kubwa ya ukuaji.

## Bidhaa Halal Malaysia zachangia 4.3% ya mauzo ya nje 2025

**Mauzo ya bidhaa za halal mwaka 2025 yalichangia asilimia 4.3 ya mauzo yote ya nje ya Malaysia, ongezeko la asilimia 0.2 kutoka mwaka uliotangulia—ikiashiria kuimarika kwa sekta hiyo katika soko la kimataifa.**

**Kwa mujibu wa Halal Development Corporation, thamani ya mauzo hayo ilifikia ringgit bilioni 68.52 (RM68.52 bilioni), ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.9 mwaka hadi mwaka licha ya changamoto za kiuchumi duniani.**

**Sekta ya vyakula na vinywaji imeendelea kuwa mhimili mkuu, ikichangia zaidi ya nusu ya mauzo yote ya halal, huku ikifuatiwa na viambato vya halal. Aidha, mafuta ya mawese na bidhaa zake yalionesha ukuaji mkubwa, yakiongeza mchango wake katika mapato ya nje.**

**Ripoti hiyo inaonyesha kuwa mahitaji ya bidhaa za halal yanaendelea kuimarika katika masoko ya kimataifa, hatua inayothibitisha nafasi ya Malaysia kama kitovu muhimu cha biashara ya halal duniani.**

## Uchumi wa Kiislamu wasifiwa kuleta ustawi wa jamii

**Waziri wa masuala ya dini wa Pakistan, Sardar Muhammad Yousaf, amesema mfumo wa uchumi wa Kiislamu unatoa suluhisho la haki katika mgawanyo wa utajiri na kupunguza ukosefu wa usawa katika jamii. Akizungumza katika Mkutano wa 6 wa Kimataifa wa Uchumi, Fedha na Benki za Kiislamu uliofanyika katika University of Management Technology, waziri huyo alisema mfumo huo si wa kifedha tu bali unazingatia maadili, uwazi na ustawi wa jamii.**

**Alibainisha kuwa uchumi wa Kiislamu unapinga unyonyaji na unahimiza shughuli halisi za kiuchumi zinazochangia maendeleo endelevu.**

**Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mfumo wa Zakat ili kurejesha imani ya wananchi na kuongeza ufanisi katika kusaidia wenye uhitaji.**

## Pakistan yazindua Sukuk ya mchanganyiko wa Ijarah, Murabaha

**Serikali ya Pakistan imefanikiwa kuzindua kwa mara ya kwanza hati ya Kiislamu ya Hybrid Sukuk, ikikusanya zaidi ya rupia bilioni 109 kupitia mnada uliovutia wawekezaji wengi kupita kiwango kilichotarajiwa.**

**Toleo hilo linatekelezwa na Idara ya Usimamizi wa Deni kwa kushirikiana na State Bank of Pakistan na Securities and Exchange Commission of Pakistan, pamoja na taasisi nyingine za kifedha. Hybrid Sukuk hiyo inaunganisha mifumo miwili ya Kiislamu—Ijarah na Murabaha.**

**Katika mfumo wa Ijarah, mali kama majengo huuzwa kwa wawekezaji na kisha kukodishwa tena, hivyo wawekezaji hupata mapato kupitia kodi badala ya riba. Kwa upande wa Murabaha, taasisi hununua bidhaa na kuziuza kwa mteja kwa bei ya juu yenye faida iliyokubaliwa mapema, badala ya kutoa mkopo wenye riba. Muundo huu mseto unalenga kuongeza uthabiti wa mapato na kuvutia wawekezaji wengi zaidi.**

**Mnada huo ulivutia zabuni zilizozidi lengo kwa mara 1.45, huku serikali ikikubali kiasi cha rupia bilioni 109.3. Viwango vya faida vilipangwa kuwa asilimia 11.80 kwa Sukuk ya mwaka mmoja na asilimia 11.7 kwa ile ya miaka 10.**

**Wataalamu wanasema hatua hiyo itaongeza imani ya wawekezaji na kupanua soko la fedha za Kiislamu, huku ikiisaidia Pakistan kupunguza gharama za kukopa kwa muda mrefu.**

## Bangladesh, licha ya Waislamu wengi; yapoteza fursa ya soko la Halal kwa Thailand

**Bangladesh, licha ya kuwa nchi yenye Waislamu wengi, inaendelea kupitwa na Thailand katika ushindani wa soko la kimataifa la halal linalokadiriwa kufikia dola trilioni 40, mojawapo ya sekta zinazokua kwa kasi duniani.**

**Ukuaji wa sekta hiyo unachochewa na ongezeko la idadi ya Waislamu duniani, inayozidi bilioni 2, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma zinazozingatia misingi ya Kiislamu. Kusini-Mashariki mwa Asia, yenye zaidi ya Waislamu milioni 240, imeendelea kuwa kitovu muhimu cha uchumi wa halal duniani.**

**Wakati Bangladesh ikikabiliwa na changamoto za urasimu, mifumo dhaifu ya uthibitishaji na ukosefu wa mkakati wa kitaifa ulioratibiwa, Thailand—nchi yenye Wabudha wengi—imewekeza kimkakati katika kujenga mfumo jumuishi wa halal unaojumuisha uzalishaji, uthibitishaji na masoko ya kimataifa.**

**KUTOKA KWA MAJIRANI**

NA MUGINI SINGIRA

# Viongozi Uganda waonya kushuka viwango vya mafunzo ya Qur'an

Viongozi wa Kiislamu nchini Uganda wameonya kuhusu kushuka kwa viwango vya ufundishaji wa Qur'an, wakisema mbinu zisizo sahihi zinaweza kupotosha maana na usahihi wa maandiko matakatifu.

Akizungumza katika hafla ya kuhitimu wahifadhi wa Qur'an katika shule za Bilal Islamic Schools, Naibu Mufti wa pili, Hafidh Muhammad Harunah Bukenya, alisema kulikuwa na nyakati ambapo wanafunzi walikuwa wakisoma aya kwa lahaja za kienyeji badala ya Kiarabu sahihi.

Alionya kuwa hali hiyo ilihatarisha uhifadhi wa Qur'an na kudhoofisha elimu ya dini. Hata hivyo, alibainisha kuwa mageuzi kupitia taasisi rasmi za Kiislamu yameanza kurejesha ubora wa ufundishaji na kuimarisha usahihi wa usomaji. Viongozi hao walisema pamoja na kuongezeka kwa wanaojiunga na programu za kuhifadhi Qur'an, kuna haja ya kuendelea kusimamia ubora wa ufundishaji.

Walitoa wito kwa walimu, wazazi na taasisi kuhakikisha mafunzo sahihi yanaendelezwa ili kulinda misingi ya elimu ya Kiislamu.



Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383



# Mvua zimeshatufunza mengi, tuchukue tahadhari

Mvua za masika zinaendelea kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini, ukiwamo Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Pwani, Iringa, Mbeya, Kagera, Geita, Njombe, Lindi, Mtwara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), mvua hizo zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya nne ya mwezi Mei na wiki ya kwanza ya mwezi Juni, 2026 katika maeneo mengi nchini.

Kama ilivyozoeleka, mvua hizo tayari zimesababisha vifo na kuharibu miundombinu muhimu ya barabara, nyumba na madaraja.

Licha ya wananchi kutahadharishwa juu ya uwezekano wa kutokea madhara hayo, inasikitisha kuona mvua hizo zinazoendelea kunyesha zimeshasababisha vifo vya watu zaidi ya 40 katika maeneo tofauti nchini, wakiwamo wanafunzi 11 wilayani Rungwe mkoa wa Mbeya.

Vifo vingine vimeripotiwa katika kata ya Segerea, wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, ambapo watoto watatu wamefariki dunia baada ya kusombwa na maji katika maeneo tofauti ya jimbo hilo.

Akizungumza bungeni Aprili 14, 2026, Mbunge wa Segerea, Agnesta Kaiza, alisema mtoto mmoja alifariki katika eneo la Kimanga, huku wengine wawili wakipoteza maisha katika eneo la Kinyerezi kufuatia mvua kubwa zilizosababisha mafuriko.

Vifo hivi huenda vingeepukika endapo hatua madhubuti za kukabiliana na hatari zinazosababishwa na mvua zingezingatiwa na kufuatwa, kama ilivyoshauriwa mapema na mamlaka husika.

Ukiachilia mbali jukumu la Serikali kufanya uokoaji katika majanga mbalimbali, wajibu wa kwanza ni watu wenyewe kuchukua tahadhari. Serikali imekuwa ikihimiza mara kwa mara watu wachukue tahadhari katika misimu ya mvua ili kuepusha majanga.

Changamoto kubwa iliyopo ni mtazamo wa baadhi ya wananchi kuchukulia mvua kama jambo la dharura, hali inayochangia kuongezeka kwa madhara pindi mvua zinaponyesha kwa wingi.

Sote tunafahamu misimu (miezi) ya mvua. Zaidi, Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini imekuwa ikitoa utabiri wa mara kwa mara unaoonesha kiwango cha mvua kinachotarajiwa pamoja na madhara yake.

Kwa msingi huo basi, tuna kila sababu ya kuchukua hatua za kukabiliana na maafa yatokanayo na mafuriko, ikiwamo vifo na magonjwa kama kipindupindu, malaria na homa ya matumbo.

Katika misimu ya mvua, jamii zilizo na huduma duni za maji safi na usafi wa mazingira ndizo huathirika zaidi. Tunadhani kwamba, moja ya njia zinazoweza kutuepusha na majanga haya ni kuwekeza katika utoaji wa elimu ya kujikinga na athari za mafuriko.

Mtazamo huo unatokana na ukweli kwamba uhai wa binadamu una thamani kubwa kuliko kitu kingine chochote duniani. Kwa kulijua hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaonya: "...wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizi." [Qur'an, 2:195].

Hivyo, tunaamini tahadhari stahiki zikichukuliwa, sambamba na kumtegemea Mwenyezi Mungu, tunaweza kubadili simulizi za maafa na kuigeuza mvua kuwa fursa ya maendeleo endelevu badala ya chanzo cha mateso ya mara kwa mara.

MAHMOUD NYAMGUMA



Familia za Wapalestina wanachota maji huko Gaza.

# Shambulio Lazua Hasira: UNICEF yailaumu Israel kwa mauaji wasambazaji misaada

Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) limesema lina "hasira kubwa" kufuatia shambulio la moto wa Israel lililowaua madereva wawili waliokuwa wamepewa kandarasi ya kusambaza maji safi kwa familia katika Ukanda wa Gaza.

Katika taarifa iliyotolewa Ijumaa, shirika hilo lilithibitisha kuwa wanaume hao waliuawa katika kituo cha kujaza maji cha Mansoura kaskazini mwa Gaza walipokuwa wakitekeleza kazi zao za kawaida za usambazaji wa maji.

Watu wengine wawili walijeruhiwa katika tukio hilo hilo.

Kituo cha Mansoura ndicho pekee kinachofanya kazi kwa sasa kwa ajili ya kujaza malori ya maji, kikiwa kimeunganishwa na mtandao wa usambazaji wa maji wa Mekorot unaohudumia Gaza City.

Kwa mujibu wa UNICEF, kituo hicho hutumika mara kadhaa kila siku kusaidia kusambaza maji kwa mamia ya maelfu ya watu, wakiwemo watoto.

Shirika hilo lilisisitiza kuwa shambulio hilo lilitokea wakati wa shughuli za kawaida bila mabadiliko yoyote ya njia au taratibu.

Shughuli Zasitishwa

Kufuatia tukio hilo, UNICEF imesema wakandarasi wameagizwa kusitisha shughuli katika eneo hilo hadi hali ya usalama itakapoimarika.

Kusitishwa huko kunahatarisha upatikanaji wa maji safi kwa sehemu kubwa ya wananchi ambao tayari wanakabiliwa na uhaba mkubwa.

UNICEF imezitaka mamlaka za Israel kufanya uchunguzi wa haraka kuhusu tukio hilo na kuhakikisha uwajibikaji kamili.

"Wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu, watoa huduma muhimu na miundombinu ya kiraia, ikiwemo vituo muhimu vya maji, kamwe hawapaswi kulengwa," ilisema taarifa hiyo.

Shirika hilo lilisisitiza kuwa ulinzi wa raia na wafanyakazi wa misaada ni wajibu wa kisheria chini ya sheria za kimataifa za kibinadamu.

Shambulio hilo linakuja wakati Gaza ikiendelea kukumbwa na mgogoro mkubwa wa kibinadamu, ambapo upatikanaji wa maji, huduma za afya na huduma za msingi bado ni mdogo sana.

UNICEF imeonya kuwa tukio hilo linaweka hatarini shughuli muhimu zinazowezesha maisha ya kila siku kwa mamia ya maelfu ya raia.

DHUL QADAH 3,

ذوالقعدة

# NASAHA ZA WIKI

0787 503 085



NA YUSUFU AMINI



# Mambo 6 ya kuzingatia kabla ya kwenda Hijja

Hijja ni ibada inayohitaji maandalizi ya kina ili itekelezwe kwa usahihi na ikubalike mbele ya Allah. Uzito wa ibada hii hauko tu katika vitendo vya nje, bali zaidi katika unyenyekevu wa ndani na nia safi ya mja.

Hivyo, maandalizi ya kimwili, kiroho na kifedha ni nguzo muhimu kwa Muislamu anayetaraji kutekeleza ibada hii adhimu. Maandalizi ya mapema yana faida kubwa, ikiwamo kupata fursa ya kusamehewa madhambi iwapo mtu atafariki kabla ya safari huku akiwa na nia ya dhati ya kuhiji.

Aidha, nia ya kweli na shauku ya kuzuru Nyumba Tukufu ya Allah (Al–Ka'aba) ni msingi muhimu, kwani Allah huwezesha yale yanayoonekana kuwa magumu kwa waja wake. Hebu sasa tuangalie mambo 6 muhimu ya kuzingatia kabla ya kuelekea katika ibada ya Hijja.

## Kwanza, elimu ya Hijja

Ni wajibu kwa hujaji kujifunza kwa kina taratibu, nguzo na masharti ya Hijja kabla ya kuanza safari.

Hii inaweza kufanyika kwa kuhudhuria semina, kusoma vitabu au kusikiliza mawaidha kutoka kwa Masheikh na wanazuoni kuhusu namna ya kutekeleza ibada ya Hijja. Hatua hii husaidia kuepuka makosa yanayoweza kuathiri ibada.

## Pili, maandalizi ya kimasurufu

Hijja ni wajibu kwa mwenye uwezo wa kifedha na siha njema, kama Allah anavyobainisha: "...na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye nyumba hiyo (Al–Ka'aba), kwa yule awezae njia ya kuendea. Na atakayekanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu." [Qur'an, 3:97].

Gharama za Hijja zinajumuisha hati ya kusafiria, tiketi, malazi na matumizi ya kila siku. Aidha, hujaji anapaswa kuhakikisha ameacha mahitaji ya kutosha kwa familia yake kabla ya kuanza safari.

## Tatu, maandalizi ya kiakili na kinafsi

Mahujaji hukumbana na changamoto mbalimbali, ikiwamo misongamano, huduma zisizoridhisha katika viwanja vya ndege ama hoteli walizofikia, au harufu mbaya kutoka kwa mtu mwingine.

Hivyo ni muhimu kuwa na subira, uvumilivu na nidhamu katika kukabiliana na changamoto zote huku wakitaraji ujira (thawabu) kutoka kwa Allah.

Haifai na ni haramu kulipiza kisasi au kumlipizia ubaya mtu aliyekufanyia ubaya, kwani hilo ni jambo linalochochea uadui na kuharibu ibada. Kuhiji kwa kufuata mafundisho sahihi ya Mtume ni muhimu ili kulinda ibada.

Allah Mtukufu anasema: "...anayekusudia kufanya Hijja katika (miezi) hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hijja hiyo..." [Qur'an, 2:197].

## Nne, usafi wa nia (Ikhlas)

Hijja yenye kukubalika ni ile inayofanywa kwa ajili ya Allah pekee bila kutafuta sifa au umaarufu (kuitwa Alhajj). Hujaji anapaswa kujiepusha na maasi na kudumisha maadili mema ya dini kipindi chote cha ibada.

## Tano, kuepuka shirk na bid'a (uzushi)

Vilevile hujaji anatakiwa aepuke vitendo vinavyoweza kuharibu tauhidi, ikiwamo kuamini vitu vinaweza kuleta manufaa au kuondoa madhara bila idhini ya Allah.

Imebainika kuwa baadhi ya mahujaji hupangusa miili yao kwa kutumia pazia zinazoifunika Al–Ka'aba au kuta za msikiti wa Makka wakidhani watapata ahueni ya matatizo yanayowakabili kama vile maradhi na shida nyinginezo. Kitendo hiki kinaweza kumuingiza mtu katika shirk.

Tuchukue mfano wa Sahaba Umar bin Khattwab (Allah amuwie radhi), ambaye alihofia kulibusu jiwe jeusi (Hajarul Aswad) lililoko katika Ka'aba wakati alipokuwa akifanya Tawafu.

Umar alisema: "Mimi nafahamu kuwa wewe ni jiwe tu ambalo halinufaishi wala kumdhuru mtu, na ingekuwa sikumuona Mtume (rehema na amani zimshukie) anakubusu, basi nisingekubusu." [Bukhari].

## Sita, matumizi bora ya muda

Mahujaji wanahimizwa kutumia muda wao katika ibada kama kusoma Qur'an, kufanya dhikri, kuomba dua, pamoja na mambo yenye manufaa kwa wengine.

Kuepuka matumizi mabaya ya muda kama kuzurura, kulala kupita kiasi au kujishughulisha sana na manunuzi ya bidhaa huchangia kuongeza thamani ya ibada.

## Nasaha muhimu

Kabla ya safari, Muislamu anapaswa kutubu kwa dhati, kurejesha haki za watu na kuomba msamaha. Toba ya kweli inahusisha kuacha dhambi, kujuta na kuazimia kutorudia tena.

MAKALA MAALUM



SHEIKH Seif Ruga 0712 690 811

# Umuhimu wa imani thabiti katika jamii ya Kiislamu

**Tatizo la jamii ya Kiislamu hivi sasa si ukosefu wa mwonekano wa kidini, uhaba wa misikiti, wala udhaifu wa mawaidha. Licha ya kuwapo kwa minara mingi ya misikiti na majukwaa ya kuhubiri, changamoto kubwa ipo katika mwonekano wa nje wa Waislamu na kukosekana kwa utekelezaji wa imani ya kweli.**
**Watu wengi wanatekeleza ibada vizuri, lakini hukosea katika upande wa muamala. Wengine hujitahidi kushikamana na Sunna za Mtume, lakini hupuuza haki na maadili. Hali hii inaonesha haja ya kujipamba na imani ya kweli itakayohuisha mwenendo wa wema waliotangulia katika kujenga utu wa muumini.**

Uislamu umeweka mizania kati ya mambo ya dhahiri na ya ndani. Ibada inapaswa kuzaa tabia njema, na tabia isiyotokana na imani sahihi haina nafasi katika Uislamu.

Allah Mtukufu anasema: "Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa hofu, na wanaposomewa Aya zake huwazidisha imani, na wanamtegemea Mola wao Mlezi." [Qur'an, 8:2]. Aya hii inaonesha kuwa imani ni hali ya moyo inayojidhihirisha kupitia matendo.

Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Hakika katika mwili kuna kipande cha nyama, kikitengemaa mwili wote hutengemaa, na kikiharibika mwili wote huharibika; nacho ni moyo." Moyo msafi huzalisha matendo mema, na moyo uliopotoka husababisha uharibifu wa matendo.

Changamoto hujitokeza pale mtu anapoonekana kutekeleza ibada kama sala na swaumu kwa nje, lakini akawa na tabia mbaya katika uhusiano na watu, au si mwaminifu katika kutekeleza haki za wengine, licha ya kutekeleza ibada kubwa. Mtume wa Allah amesema: "Huenda mfungaji akawa hana anachopata isipokuwa kushinda na njaa; na huenda anayesimama kusali usiku akawa hana anachopata isipokuwa kukesha tu." Hadith hii inasisitiza umuhimu wa kuwa na nia safi kwa Allah katika ibada na kuhakikisha zinaleta mabadiliko chanya katika maisha ya kila siku.

## Kwa nini hali hii?

Zipo sababu kadhaa zinazochangia dini kubaki katika mwonekano wa nje bila kuleta matokeo ya imani ya kweli.

## Kwanza, udhaifu katika kujifunza elimu ya sharia

Kujifunza elimu ya dini ni ibada ya lazima (faradhi). Kuipuuza ni kujinyima fursa ya daraja ya juu mbele ya Allah. Qur'an inasema: "Mwenyezi Mungu atawainua walioamini miongoni mwenu, na waliopewa elimu daraja za juu..." [Qur'an, 58:11].

## Pili, udhaifu katika kuitakasa nafsi

Allah anasema: "Hakika amefaulu yule aliyetakasa nafsi yake." [Qur'an, 91:9]. Hata hivyo, suala la utakaso wa nafsi halijapewa uzito unaostahili katika khutba na mihadhara mingi, tofauti na msisitizo uliokuwepo katika zama za wema waliotangulia (Salaf Swalih).

Utakaso wa nafsi unapaswa kufanywa kwa kufuata mwongozo wa Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie). Ibn Qayyim (Allah amrehemu) anasema: "Utakaso wa nafsi ni mgumu zaidi kuliko kutibu mwili. Anayejitibu kwa mbinu zake binafsi anaweza kushindwa..."

## Tatu, kuzingatia dhahiri ya jambo kuliko malengo

Baadhi ya watu hujikita katika taswira ya nje ya ibada na kusahau malengo yake ya msingi kama Ikhlasi, ukweli na huruma. Mtume amesema: "Hakika matendo huzingatiwa kwa nia, na kila mtu atalipwa kulingana na alivyokusudia." [Bukhari na Muslim]. Bila nia ya kweli ibada haiwezi kustawi.

## Nne, kasoro katika mihadhara ya ulinganiaji

Baadhi ya mihadhara imevuka mipaka kwa ukali wake kutokana na ushadadiaji (ghuluw) hivyo kuwaogopesha watu, na mingine imepunguza msisitizo na kupelekea udhaifu katika kufuata amri za dini.

Allah anasema: "Enyi Watu wa Kitabu! Msipinduke mipaka katika dini yenu, wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lililo la kweli...." [Qur'an, 4:171]. Mfumo wa wema waliotangulia (Salaf Swalih) katika kujenga imani unalenga kuunda utu wa muumini kwa msingi wa uwiano kati ya imani na tabia, elimu na vitendo, na ibada na maadili.

Imani si maneno tu, wala si elimu isiyo na matokeo; ni lazima ionekane katika moyo, maneno na vitendo. Tauhidi (kumpwekesha Allah) ndiyo msingi wa dini, na wajibu wa kwanza kwa Muislamu ni kumwabudu Allah peke yake.

Hii ndiyo njia ya Manabii wote, kama Allah Ta'ala anavyosema: "Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi; basi niabuduni Mimi tu." [Qur'an, 21:25].

## Kumfuata Mtume

Bila kumfuata Mtume Muhammad (rehema na amani ya Mwenyezi Mungu zimshukie) dini haiwezi kustawi, kwani kumtii Mtume ni sehemu ya kumtii Mwenyezi Mungu. Aidha, kufuata mwenendo (Sunna) wake ni njia sahihi ya uongofu na kuupuuzia ni kufungua mlango wa uzushi (bid'a).

Mtume amesema: "Shikamaneni na mwenendo wangu na mwenendo wa Makhalifa waongofu." Mfumo huu unaweka msingi wa imani sahihi inayomjenga mtu na kuifanya jamii kuwa na maadili mema.

ذُو القِعدة

KALAMU HURU

SEHEMU YA 5

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Swala, nguzo ya maisha ya Muislamu baada ya Ramadhan

Miongoni mwa mambo makubwa ambayo Muislamu huyaimarisha sana ndani ya mwezi wa Ramadhan ni swala. Ndani ya mwezi huo mtukufu, misikiti ilijaa waumini, safu zilisimama kwa unyenyekevu, na watu walijitahidi sana kutekeleza swala tano kwa wakati pamoja na swala za sunna kama vile Tarawehe na Qiyamu-l-Layl, n.k.

Hali ile ilionesha wazi kwamba Ramadhan ni shule ya kurekebisha uhusiano kati ya mja na Mola wake Mlezi kupitia swala. Lakini swali muhimu ni hili: je, baada ya Ramadhan kuisha, swala zetu na ibada nyingine zinaendelea kuwa na ubora ule ule?

Swala ni nini katika maisha ya kila siku ya Muislamu? Ni nguzo kuu na himilivu ya Uislamu baada ya shahada. Ni kiungo cha moja kwa moja kati ya mja na Mwenyezi Mungu. Ndani yake, Muislamu husimama mbele ya Mola wake Mlezi, humtukuza, humshukuru, na kumuomba msaada.

Swala si ibada ya kawaida; ni msingi wa maisha ya Muislamu. Ikiwa swala itadumishwa na kusimamishwa vizuri, basi maisha mengine ya mtu pia yatasimama vizuri. Ndiyo maana swala inatajwa kuwa ni kizuizi dhidi ya maovu na mambo machafu.

Ndani ya Ramadhan, Muislamu alijenga tabia ya kuswali kwa wakati. Wengi waliacha kuchelewesha swala, na badala yake walijitahidi kuswali kwa wakati na kwa unyenyekevu (khushuu). Pia, waliswali kwa wingi zaidi kuliko kawaida, hasa nyakati za usiku.

Lakini changamoto imeanza kujitokeza baada ya Ramadhan. Watu wengi wamerudi katika hali yao ya zamani: kuchelewesha swala, kuacha baadhi ya swala, au kuswali bila kuzingatia unyenyekevu. Hii inaonesha kuwa huenda mafunzo ya Ramadhan hayakutuathiri au hayakudumu ipasavyo.

Muislamu anapaswa kuelewa kwamba swala si ya Ramadhan tu, bali ni wajibu wa kila siku katika maisha yake yote.

Kama alivyoweza kuswali kwa nidhamu ndani ya Ramadhan, basi ana uwezo wa kufanya hivyo hata baada ya Ramadhan.

Miongoni mwa njia za kudumisha swala baada ya Ramadhan ni kuweka kipaumbele katika maisha. Mtu anapaswa kupanga shughuli zake kulingana na swala, si kupanga swala kulingana na shughuli zake. Hii itamsaidia kuwa na nidhamu ya kweli katika ibada hii muhimu.



Aidha, ni muhimu kuendeleza kuswali kwa jamaa msikitini kwa wanaume, kwani hii huongeza hamasa na kusaidia kudumisha uthabiti. Kwa wanawake, kuswali kwa wakati na kwa utulivu nyumbani, na hata msikitini, pia ni jambo lenye thamani kubwa.

Vilevile, Muislamu anatakiwa kujitahidi kuboresha ubora wa swala yake, si tu kuitekeleza. Hii ni pamoja na kuelewa anachokisoma, kuwa na khushuu, na kujiepusha na mambo yanayomtoa katika umakini wakati wa swala.

Moja ya njia za kuongeza khushuu ni kujikumbusha kwamba unasimama mbele ya Mwenyezi Mungu. Ukifanya hivyo, swala haitakuwa tena ni jukumu la kuripua au kumaliza kwa haraka, bali itakuwa ni wakati wa kipekee wa kuzungumza na Mola wako Mlezi.

Pia, kuendelea na swala za sunna baada ya Ramadhan ni njia nzuri ya kulinda swala za faradhi. Ibada za sunna husaidia sana kuziba mapungufu na kuimarisha uhusiano wa mja na Allah.

Kwa hakika, swala ni nuru ya maisha ya Muislamu. Inamleta karibu na Mwenyezi Mungu, inamtuliza moyo, na inamkinga dhidi ya maovu. Mtu anayeshikamana na swala hatapotea kirahisi katika maisha.

Hivyo basi, mafanikio tuliyoyapata katika Ramadhan yanapaswa kuonekana katika namna Muislamu anavyodumisha swala zake baada ya mwezi huo mtukufu kuondoka. Ikiwa swala imara itaendelea, basi hiyo ni dalili njema ya kukubaliwa kwa ibada zake.

Lakini pamoja na swala, kuna ibada nyingine muhimu sana ambayo Ramadhan huijenga kwa kina ndani ya moyo wa Muislamu—nayo ni kutoa sana sadaka na kuwasaidia wengine.

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Sadaka na Ukarimu – Roho ya Kijamii Baada ya Ramadhan, na jinsi ya kuendeleza tabia ya kutoa tuliyojifunza ndani ya mwezi mtukufu.

ذو القعدة

# فتاوى



# Je kuna zaka ya mshahara?

**Swali: Naomba kufahamishwa: Je, kuna zaka ya mshahara wa mfanyakazi kwa kila mwezi?**

**Jibu:** Haimuwajibikii mtu kutoa zaka kutokana na mshahara wa kila mwezi; kwa sababu zaka huwa ni wajibu baada ya kupita mwaka mzima (hawl) na juu ya mali iliyofikia nisabu.

Utaratibu wa kulipwa mshahara kila mwezi ni mfumo tu unaotumika katika baadhi ya nchi, ilhali katika sehemu nyingine watu hulipwa kila wiki au hata kila siku. Hivyo, si sahihi kusema kuwa kila kipato cha kila mwezi, wiki au siku kinawajibikiwa zaka moja kwa moja.

Mfumo wa zaka unategemea kupita mwaka mzima (hawl) juu ya mali iliyobaki. Ikiwa mfanyakazi ataweza kubakiza sehemu ya mshahara wake—baada ya kugharamia mahitaji muhimu ya familia—na kiasi hicho kikafikia nisabu, kisha kikakaa kwa mwaka mzima bila kupungua chini ya kiwango hicho, basi hapo zaka itawajibika.

Imepokewa katika hadithi kutoka kwa Bi Aisha (Allah amridhie) kwamba Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna zaka katika mali mpaka ipite juu yake mwaka mzima." [Ibn Majah na wengineo].

Hata hivyo, hakuna ubaya kwa mtu kutoa sadaka ya mshahara wake kila mwezi kwa hiari, kama njia ya kujikurubisha kwa Allah na kusaidia wahitaji, lakini si wajibu wa kisheria.

Masharti ya zaka ni haya yafuatayo: Uislamu, uhuru, kumiliki nisabu (kiasi cha chini kinachowajibisha zaka), kupita mwaka mzima (hawl) na mali kuwa ya kukua (ina uwezo wa kuongezeka au kuleta faida).

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Kuna mfanyakazi anaweka akiba kutoka kwenye mshahara wake kila mwezi kiasi cha fedha kinachotofautiana; mwezi mmoja anaweka kidogo, mwezi mwingine anaweka zaidi. Baadhi ya fedha hizo zimekaa kwa mwaka mzima (zimefikia muda wa kutoa zaka), na nyingine bado hazijafikisha mwaka. Pia hajui ni kiasi gani aliweka kila mwezi. Basi atatoaje zaka? Mfanyakazi mwingine hupokea mshahara wake kila mwezi na huweka fedha zote anazopokea kwenye akaunti au hazina yake. Kisha hutumia kutoka humo kila siku au kwa vipindi vya karibu kwa matumizi ya nyumbani na mahitaji mengine, kwa kiasi kinachotofautiana kulingana na haja. Je, muda wa mwaka (hawl) wa fedha zilizobaki kwenye akaunti hiyo huhesabiwaje? Na zaka hutolewaje katika hali kama hii, ilhali akiba hiyo si yote iliyokaa mwaka mzima?**

**Jibu:** Kwa kuwa swali la kwanza na la pili yana maana moja na yana mifano mingine inayofanana nayo, nimeona nijibu kwa jibu la jumla ili faida iwe pana:

Yeyote anayemiliki kiwango cha chini cha zaka (nisabu) cha fedha, kisha akapata fedha nyingine kwa vipindi tofauti, ambazo hazikutokana na zile za kwanza wala hazikuzaliwa kutokana nazo, bali ni fedha huru kama vile akiba ya mshahara wa mfanyakazi kila mwezi, au urithi, au zawadi, au mapato ya kodi ya nyumba, basi inampasa ajipangie utaratibu wa hesabu.

Kwa maana nyingine, ikiwa anataka kuwa makini sana katika haki yake na kuhakikisha kuwa hatoi kama sadaka isipokuwa kile kilichowajibika kwake kama zaka tu, basi aweke kumbukumbu ya mapato yake, na kila kiasi cha fedha kiwe na mwaka wake (hawl) unaoanza tangu siku alipokimiliki. Kisha, atoe zaka ya kila kiasi peke yake kila kinapofikisha mwaka tangu alipopata.

Lakini ikiwa anataka urahisi na kuchukua njia ya wepesi, na moyo wake uwe tayari kuwapa kipaumbele maskini na walengwa wa zaka kuliko nafsi yake, basi atoe zaka ya fedha zote alizonazo mara tu mwaka unapofika kwa ile nisabu ya kwanza aliyomiliki.

Njia hii ina malipo makubwa zaidi, daraja la juu zaidi, inaleta urahisi zaidi, na inalinda haki za maskini na walengwa wengine wa zaka. Kiasi chochote kitakachozidi kile kilichofikisha mwaka kitahesabiwa kama zaka ya mapema kwa mali ambayo bado haijafikisha mwaka.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Na Said Rajab
0783 650 803

# Kauli za Trump zinapofichua ubaradhuli wa Marekani

Hivi karibuni, Rais wa Marekani, Donald Trump alitishia kuishambulia Iran kwa mabomu na kuirudisha katika zama za mawe iwapo haitaufungua Mlango–Bahari wa Hormuz. Kauli hiyo ilirudiwa pia na Waziri wake wa Ulinzi, Pete Hegseth.

Hakika sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, aliyemuangamiza Firauni na wenzake na kuangusha dola na himaya mbalimbali kutokana na kiburi chao.

Mafirauni wa zama hizi wanaonekana kutojifunza kutokana na historia, licha ya kurejea mara kwa mara kauli kuhusu "zama za mawe" katika matamshi yao yaliyojaa chuki na kiburi.

Kauli za Trump dhidi ya Iran zinaakisi mtindo wa muda mrefu katika historia ya kijeshi ya Marekani, ambapo matumizi ya nguvu kubwa na vitisho vya maangamizi vimekuwa chombo cha kufikia malengo ya kisiasa.

Nchini Iraq, Marekani ilifanya mashambulizi mengi ya kijeshi yaliyoharibu miundombinu ya kiraia, kuanzia Vita vya Ghuba vya mwaka 1991 hadi mashambulizi makubwa ya mabomu ya mwaka 2003, uvamizi na hatimaye ukaliaji wa kijeshi.

Shule, hospitali, mitambo ya umeme na mifumo ya maji viliharibiwa na kuwaacha mamilioni ya wananchi wakiwa wakimbizi pamoja na kuzalisha migogoro ya muda mrefu ya kibinadamu.

Kadhalika, nchini Afghanistan, miongo kadhaa ya migogoro kufuatia uvamizi ulioongozwa na Marekani mwaka 2001 ilihusisha kampeni kubwa za mabomu zilizolenga watu bila ubaguzi na kusababisha vifo vya raia wengi wasio na hatia pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya miji, vijiji, shule na vituo vya afya.

Mtindo huu una mizizi ya muda mrefu zaidi kihistoria. Wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Marekani ilifanya kampeni kubwa za mashambulizi ya mabomu katika miji ya Tokyo, Osaka na Toyama nchini Japan kwa lengo la kuharibu miundombinu ya kiraia.

Baadaye ilitumia mabomu ya atomiki huko Hiroshima na Nagasaki na kuangamiza raia wengi kwa madai ya kuharakisha kumaliza vita.

Nchini Vietnam, vikosi vya Marekani vilifanya kampeni endelevu za mabomu katika maeneo ya Kaskazini na Kusini, ikiwa ni pamoja na operesheni ya 'Rolling Thunder' kwa lengo la kubomoa miundombinu, hali iliyosababisha vifo vingi vya raia na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Ukiacha Asia na Mashariki ya Kati, Marekani pia ilihusika katika uingiliaji wa kisiasa na kijeshi katika Amerika Kusini, ikiwemo mapinduzi nchini Chile na Guatemala, pamoja na kusaidia makundi ya waasi.

Hali hii ilichangia kwa kiasi kikubwa kukosekana kwa utulivu wa kijamii na kiuchumi kwa muda mrefu.

Katika kanda zote hizo, mkakati wa kutumia nguvu kubwa za kijeshi na kuvuruga maisha ya raia umeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kutekeleza malengo ya kijiografia na kisiasa ya Marekani, huku ukisababisha madhara ya kibinadamu yanayoendelea hata baada ya vita kuisha.



Tofauti na vitisho vya awali vya kijeshi ambavyo vilifunikwa kwa hoja za kulinda raia, kukuza demokrasia au kupinga udhalimu, matamshi ya sasa ya Marekani dhidi ya Iran yamekuja wazi bila kujificha nyuma ya visingizio hivyo. Hivi sasa lugha imekuwa ya wazi zaidi. Ahadi ya Trump ya kuishambulia Iran na kuirudisha katika zama za mawe inaonesha wazi sura ya sera ya Marekani inayohusishwa na vurugu na uharibifu, ambayo hapo awali ilikuwa ikifichwa kwa hoja mbalimbali.

Marekani haifichi tena uwezekano wa kutumia nguvu zake kwa njia zenye madhara makubwa kwa jamii. Kauli za Trump zinachukuliwa kama ushahidi wa mwelekeo huo.

Kwa kumalizia, dunia inaendelea kutafuta mfumo mbadala usioegemea katika ubabe au maslahi ya faida pekee, bali unaozingatia haki, ustawi na huruma ya kweli – mambo ambayo mfumo wa sasa wa kibepari unaonekana kushindwa kuyaondoa kikamilifu.

Wakati mataifa makubwa yakionesha nguvu zao na kusherehekea uharibifu, wananchi wa kawaida wanaendelea kubeba athari za hali hiyo, wakitamani mfumo wa uongozi unaothamini utu, heshima na thamani ya maisha ya binadamu.

Utulivu wa kweli na amani ya kudumu vinatokana na mfumo unaolinda maisha, kudumisha haki na kuonesha huruma, kama ulivyowekwa na Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anauliza: "Je, hawatembei katika ardhi wakaona vipi ilikuwa hatma ya wale waliokuwa kabla yao? Hao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao na athari katika nchi, lakini Mwenyezi Mungu aliwakamata kwa sababu ya madhambi yao, na wala hawakuwa na wa kuwalinda dhidi ya Mwenyezi Mungu." [Qur'an, 40:21].

DHUL QADAH 3,

ذوالقعدة

MAKALA MAALUM

Na Zaharani Baraka

# Kuna faida nyingi ukitoa sadaka ya kudumu



**Katikati ya mji wa Madina kuna kisima chenye maji matamu kiitwacho 'Bi'ir Ruma', ambacho Sahaba mtukufu, Uthman bin Affan (Allah amridhie) alikifanya kuwa wakfu (sadaka ya kudumu) kwa Waislamu wa zama zake na vizazi vilivyofuata.**

**Kisima hicho kipo upande wa Kaskazini Magharibi mwa mji wa Madina, karibu na bonde la Wadi al–Aqiq, na hadi leo hutembelewa na watu wengi wanaopenda historia ya Kiislamu. Eneo hili linabeba kielelezo cha tukio mojawapo bora kabisa la wakfu katika Uislamu.**

## Simulizi ya kisima hiki

Kisima cha Bi'ir Ruma kinachojulikana pia kama Bi'ir Uthman ni kisima cha kihistoria katika mji wa Madina. Khalifa Uthman bin Affan (Allah amridhie) alinunua sehemu ya kisima hicho kutoka kwa Myahudi aliyekuwa akiishi Madina ili kiwe mali ya Waislamu.

Katika miaka ya mwanzo ya Hijra, Waislamu walikabiliwa na uhaba mkubwa wa maji, hali iliyowalazimu kununua maji kwa gharama kubwa kutoka katika kisima hicho.

Mtume (rehema na amani zimshukie) aliwahamasisha kwa kusema: "Ni nani atakayenunua Bi'ir Ruma na kuwafanya Waislamu watumie maji yake, naye atapata kwa hilo chemchem Peponi?"

Uthman alikubali wito huo na kutumia fursa hiyo, akanunua nusu ya kisima kwa dirham 12,000 na kuifanya sehemu hiyo kuwa sadaka kwa Waislamu. Matumizi ya kisima yalipangiliwa kwa zamu, ambapo siku moja yalikuwa kwa Waislamu na siku nyingine kwa mmiliki wa awali, Myahudi.

Baadaye, mmiliki huyo alipoona Waislamu wanapata manufaa makubwa alimuuzia Uthman sehemu iliyobaki kwa dirham 8,000, naye akaifanya kuwa wakfu kwa Waislamu.

Awali, kisima hiki kilimilikiwa na mtu kutoka kabila la Muzaynah, kisha kikarithiwa na Ruma Al–Ghifari, na baadaye kikamilikiwa na Myahudi aliyekuwa anawauzia Waislamu maji.

Kisima hiki chenye baraka kimeendelea kuwa chanzo endelevu cha thawabu tangu kiliponunuliwa na Uthman na baadaye kukabidhiwa kwa Waislamu, hatua inayokifanya kuwa alama ya kudumu ya kujitolea na mojawapo ya vielelezo muhimu vya kihistoria vinavyohusishwa na Masahaba.

## Hali ya sasa ya Bi'ir Ruma

Kwa sasa, serikali ya Saudi Arabia imekikarabati kisima hiki na kulitunza eneo lake kwa kupanda miti ya mitende na kugawa matunda yake kwa wahitaji. Hivyo, sadaka ya Uthman bin Affan inaendelea kutoa manufaa hadi leo, ikiwa ni mfano halisi wa sadaka yenye kuendelea (sadaka jariyah).

Mtume (rehema na amani zimshukie) amehimiza kutoa sadaka zenye manufaa ya kudumu. Hii ni aina ya sadaka ambayo, baada ya mja kufa huendelea kumletea thawabu. Mfano wake ni ule wa Uthman (Allah amridhie), ambaye anaendelea kuvuna thawabu za sadaka yake kwa zaidi ya karne 14.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Anapokufa mwanadamu matendo yake hukatika isipokuwa mambo matatu: sadaka yenye kuendelea, elimu yenye manufaa, au mtoto mwema anayemuombea dua." [Muslim].

Sadaka yenye kuendelea ni kama kuchimba kisima, kujenga msikiti au kusaidia jambo linaloendelea kuwafaidisha watu. Elimu yenye manufaa ni kama kufundisha Qur'an au maarifa mema, na mtoto mwema ni yule anayemuombea mzazi wake dua.

Faida za sadaka yenye kuendelea ni nyingi, ikiwamo kuwekeza kwa ajili ya Akhera, ambapo akiba ya matendo mema huendelea hata baada ya kifo. Uwekezaji huu ni rasilimali isiyochakaa wala kupoteza thamani.

Kutowekeza katika sadaka ya kudumu ni kujikosesha fursa ya kupata kheri za Akhera na hata za duniani. Bila ya kufanya hivyo, mja hukosa chanzo cha ujira endelevu, na baada ya kufa matendo yake hukatika kabisa.

## Kusimama kwa mizani ya mema

Kukosa sadaka yenye kuendelea hupunguza fursa ya kuongeza uzito wa mizani ya mema Siku ya Kiyama, ambapo hakuna kitakachomnufaisha mja isipokuwa matendo yake mema aliyofanya duniani.

Sadaka kama kuchimba kisima, kujenga msikiti au kusaidia watu kupata elimu huleta manufaa ya muda mrefu kwa jamii. Kutojihusisha na mambo haya ni kujinyima malipo ya kuwasaidia watu baada ya kifo chako.

Msaada wa mtu, kipaji chake na huduma yake hukoma mara tu anapofariki, isipokuwa pale anapokuwa ameweka msingi wa sadaka ya kudumu. Miongoni mwa manufaa yake, pia ni kukumbukwa na kutajwa vyema na jamii hata baada ya kifo.

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803



# Athari ya vita vya Iran kwa umma wa Kiislamu

**Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulihitimisha kwa kusisitiza kuwa Muislamu haruhusiwi kufurahia Iran kushambuliwa kwa mabomu na Marekani na Israel, bila kujali makosa ya utawala wa nchi hiyo, kwani kitendo hicho husababisha uharibifu katika ardhi ya Waislamu. Ndugu msomaji, katika sehemu hii ya mwisho tunaendelea kuchambua athari nyingine zitokanazo na vita vya Iran kwa umma wa Kiislamu. *Sasa endelea...***

Uchokozi wa Marekani na Israel dhidi ya Iran hauilengi Iran pekee, bali unakusudia kudhoofisha eneo zima la Mashariki ya Kati na kuliweka chini ya ushawishi wao.

Marekani inalenga kuimarisha udhibiti wake katika eneo hilo, kuanzisha ukiritimba juu ya rasilimali za Waislamu na kulazimisha mfumo wake potofu wa maisha kwa jamii hiyo.

Kinachoendelea Iran ni sehemu ya marekebisho ya kimkakati ya Marekani katika hesabu zake za kikanda, ikiwa ni pamoja na jitihada za kubadili utawala wa Iran kutoka kuwa dola inayozunguka kwenye ushawishi wake hadi kuwa taifa kibaraka linalofuata sera za Marekani.

Hata hivyo, utawala wa Iran umekuwa ukipinga shinikizo hilo, hasa katika masuala ya ndani kama urutubishaji wa madini ya urani na kuimarisha uwezo wake wa kiulinzi kupitia utengenezaji wa makombora ya kisasa.

Pamoja na hayo, uadui dhidi ya utawala wa Iran haupaswi kuwa sababu ya kuhalalisha au kushabikia uchokozi wa Marekani na Israel dhidi yake. Aidha, utawala wa Iran – kama zilivyo tawala nyingine katika Mashariki ya Kati una changamoto zake.

Hata hivyo, tofauti zetu na hasira dhidi ya Iran hazipaswi kufungua mlango wa kuvamiwa kwa ardhi ya Waislamu na kuiacha katika hatari ya kudhibitiwa na Marekani na Mayahudi.

Yeyote mwenye uelewa wa kisiasa na mtazamo wa uhalisia, anaelewa kuwa ushindi wa Marekani na Israel dhidi ya Iran utakuwa na madhara makubwa.

Dola ghasibu ya Kiyahudi, inayosababisha ghadhabu za Mwenyezi Mungu itazidi kuimarika huku uchokozi wa Marekani katika eneo la Mashariki ya Kati ukizidi kushamiri

Matokeo yake yatakuwa mabaya zaidi kwa Waislamu, yakifungua mlango wa kuwafanya kuwa chini ya nguvu za mataifa ya kigeni, pamoja na kuhatarisha heshima yao, matukufu yao na maeneo yao matakatifu.

Kwa upande mwingine, kuchochea mzozo kati ya Sunni na Shia katika wakati huu kunamnufaisha zaidi kafiri anayepigana na Waislamu, ambaye hatofautishi kati ya Sunni na Shia katika uadui wake.

Allah Mtukufu anasema: "Hao ni watu waliopita. Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakayoyachuma, wala nyinyi hamtaulizwa waliyokuwa wakiyafanya wao." [Qur'an, 2:134].

Hii ndiyo kanuni inayopaswa kuwaongoza Waislamu – kuacha migogoro ya kale na kuzingatia wajibu wao wa sasa. Kila Muislamu anawajibika kwa Mwenyezi Mungu – ama kuendeleza mgawanyiko au kuushinda.

Mfano bora unapatikana katika maisha ya Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie), alipokemea ukabila wa zama za jahiliya uliokuwa ukigawa jamii na kuchochea migogoro. Mtume alisema: "Je, mnalingania ujahili ilhali bado nipo nanyi?" Badala yake, Mtume aliasisi jamii iliyojengwa juu ya misingi ya imani na umoja wa umma.

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama




# Matumizi ya AI katika tafiti za kitaaluma: Msaada au mbadala?

Katika mjadala wa sasa kuhusu akili bandia (AI) katika taaluma, hoja kuu si kama teknolojia hii ni muhimu, bali ni jinsi inavyopaswa kutumika. Ushahidi kutoka kwa wataalamu wa uandishi wa kitaaluma na taasisi za elimu unaonyesha msimamo mmoja thabiti: AI ni zana ya kusaidia utafiti—siyo mbadala wa fikra za msomi.

Kwanza, ni muhimu kuelewa nafasi halisi ya AI katika mchakato wa utafiti. Kwa mujibu wa mwongozo wa University of Pretoria, AI inapaswa kusaidia kazi za maandalizi kama kupanga mawazo, kuchuja taarifa na kuelewa dhana ngumu.

Hizi ndizo zinazoitwa "kazi zisizoonekana"—yaani hatua za nyuma ya pazia zinazorahisisha utafiti, lakini si sehemu ya mchango wa kiakili unaotakiwa kutoka kwa mtafiti. Kwa maneno mengine, AI inaweza kukusaidia kufika mezani, lakini haiwezi kula kwa niaba yako.

Katika hatua za awali, AI inaweza kuwa muhimu sana katika kuboresha mada ya utafiti, kupendekeza maeneo mapya ya uchunguzi au kutoa muhtasari wa awali wa maandiko marefu. Hata hivyo, wataalamu wanasisitiza tahadhari: muhtasari wa AI hauwezi kuchukua nafasi ya kusoma chanzo halisi. Uhakiki wa kina na uchambuzi wa kitaaluma bado ni jukumu la mtafiti mwenyewe.

Kwa upande mwingine, mjadala wa kisasa umeenda hatua moja mbele zaidi—kuangalia jinsi AI inaweza kuboresha ubora wa uandishi wa kitaaluma. Katika uchambuzi uliowasilishwa na wataalamu wa uandishi kupitia Lumivero, hoja kuu ni kwamba AI inafanya kazi vizuri zaidi pale inapoongeza uwezo wa mtafiti, si pale inapojaribu kuchukua nafasi yake.

Mbinu moja iliyopendekezwa ni kile kinachoitwa "AI sandwich." Hapa, AI hutumika mwanzoni kusaidia kupanga mawazo au kuunda muhtasari, kisha mtafiti huandika rasimu kwa juhudi zake binafsi, na hatimaye hurudi kutumia AI kwa maoni ya marekebisho. Mfumo huu unahakikisha kuwa umiliki wa mawazo unabaki kwa mtafiti huku akitumia nguvu ya AI kuboresha uwazi na mtiririko wa hoja.

Aidha, AI inaweza kusaidia katika eneo gumu zaidi la uandishi wa kitaaluma: synthesis—yaani kuunganisha tafiti mbalimbali ili kutoa hoja mpya. Badala ya kunukuu au kufupisha tafiti moja baada ya nyingine, mtafiti anatakiwa kubaini mifumo, tofauti na mapungufu katika maandiko. AI inaweza kusaidia kwa kubainisha mada zinazojirudia au kulinganisha hoja, lakini tafsiri ya mwisho inabaki kuwa ya kibinadamu.

Hapa ndipo mstari wa maadili unapochorwa wazi. AI inaweza kusaidia katika kupanga, kuchambua na hata kupendekeza hoja mbadala, lakini haiwezi—na haipaswi—kuchukua nafasi ya uamuzi wa kitaaluma.

Kwa mfano, kutumia AI kuibua hoja pinzani kunaweza kuimarisha utafiti kwa kumsaidia mtafiti kutazama mada kutoka pande tofauti. Lakini hoja hizo lazima zithibitishwe kupitia vyanzo halisi vya kitaaluma.

Kwa mtazamo mpana zaidi, wataalamu wanapendekeza kufikiria AI kama "msaidizi wa utafiti mwenye mipaka." Anaweza kupanga faili, kutoa muhtasari au kupendekeza mwelekeo—lakini hawezi kufanya uchambuzi wa kina au kuandika kazi ya mwisho kwa uadilifu wa kitaaluma.

Hitimisho linabaki kuwa la tahadhari lakini lenye matumaini. AI inaweza kuboresha kasi na ubora wa uandishi wa kitaaluma, lakini tu pale inapotumika kwa makusudi na kwa nidhamu ya kitaaluma.

Inapochukuliwa kama mbadala wa fikra za msomi, matokeo yake huwa ni kazi dhaifu na isiyo na uhalisia. Lakini inapochukuliwa kama mshirika wa kufikiri, inaweza kusaidia watafiti kuandika kwa uwazi zaidi, kuhoji kwa kina zaidi na kuchangia kwa nguvu zaidi katika mijadala ya kitaaluma.

Kwa kifupi, mustakabali wa utafiti hauko katika kuchagua kati ya binadamu na mashine, bali katika kujifunza jinsi ya kuzifanya zifanye kazi pamoja bila kupoteza kiini cha utafiti: fikra huru na hoja makini.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 4



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Wiki iliyopita katika mfululizo wa makala hii tulijifunza kuwa Nabii Musa (amani ya Allah iwe juu yake), akiwa kijana mwenye nguvu, alimuua jamaa wa Kikibtwi kimakosa. Akamuomba msamaha Mola wake, naye akamsamehe. Musa alimuahidi Mola wake kuwa hatokuwa tena msaidizi wa watu madhalimu.**

**Tukio hili lilimfanya Musa kuwa na wasiwasi mkubwa kwani alijua kwamba, pindi ikibainika kuwa yeye ndiye aliyemuua yule mtu na kupatikana naye, atauawa. Lakini katika hali isiyotarajiwa, siku ya pili akamkuta jamaa yake yule anagombana na mtu mwingine na kumuomba tena amsaidie.**

**Hii inatupa funzo kwamba kuna baadhi ya watu wanapenda sana ugomvi na kuanzisha migogoro ya kukosana na watu, kisha kuwahusisha watu wasiohusu.**

**Tusome aya ifuatayo: "Akapambazukiwa mjini na asubuhi (siku ya pili) akiwa na hofu (kubwa), anangoja (lipi litamfika kwa yale yaliyotokea jana), mara yule aliyemuomba msaada jana tahamaki anamwita (amsaidie kupigana na adui yake mwingine). Musa akamwambia, 'Bila shaka wewe ni mpotofu uliye dhahiri (kila siku huishi kugombana na watu).' Basi alipotaka kumtia mkononi yule adui yao (yule aliyeomba msaada alidhani kuwa Musa anataka kumpiga yeye sasa kwa yale maneno aliyoyatanguliza kuyasema), akasema: 'Ewe Musa, unataka kuniua kama ulivyomuua yule mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi, wala hupendi kuwa miongoni mwa watu wazuri (wasuluhishi).'" [Qur'an, 28:18–19]**

**Basi ikafahamika: alaa! Kumbe Musa ndiye aliyemuua mtu, na habari yake ikaenea mji mzima.**

### Fir'aun aagiza Musa akamatwe

Ndipo Fir'aun akatoa agizo la Musa kutafutwa, akamatwe popote alipo na auliwe. Hapo hofu ya Musa juu ya kuuawa ikazidi, na kuanza kujificha zaidi mbali na mji na mikusanyiko ya watu.

"Penye waovu wengi pana wema, japo wachache." Musa (amani ya Allah iwe juu yake) alipata msamaria mwema aliyemfuata aliko na kumpa habari za mjini kwamba anatafutwa auawe. Alimtahadharisha na kumuomba bora atoke Misri kwa usalama wake. Jina la mtu yule halikutajwa katika Qur'an.

Tuirejee tena Qur'an: "Basi akaja mtu (fulani) kutoka mwisho wa mji akikimbia mbio, akasema, 'Ewe Musa, wakubwa wanashauriana juu ya kukuua; basi ondoka (katika nchi hii). Bila shaka mimi ni miongoni mwa wanaokutakia mema.'" [Qur'an, 28:20].

### Musa aondoka Misri

Basi kweli, Musa aliifanyia kazi nasaha ya yule mtu, na kwa mara ya kwanza alitoka nchini kwake na kukimbia.

"Basi Musa akatoka huku anaogopa na kungojea (lipi litamtokea), akasema, 'Mola wangu, niokoe na (shari za) watu madhalimu.'" [Qur'an, 28:21]. "Na alipoelekea upande wa Madyan, alisema, 'Asaa Mola wangu ataniongoza njia ya sawa.'" [Qur'an, 28:21–22].

### Musa awasaidia mabinti wawili

Musa (amani ya Allah iwe juu yake) alifuata njia iliyomuelekeza nchi iliyojulikana kwa jina la Madyan. Kwa mujibu wa Qur'an, Madyan ni nchi aliyoishi Mtume Shu'ayb (amani ya Allah iwe juu yake).

Allah Mtukufu anasema: "Na alipofikia maji ya Madyan (mahala walipoteka maji watu wa mji huo), alikuta kundi (kubwa) la watu wananywesha (wanyama wao maji), na akakuta kando yao wanawake wawili wanawazuia (wanyama wao wasiende kunywa pamoja na wengine). Akasema, 'Mna nini nyinyi? (Mbona hamteki maji?)' Wakasema, 'Hatunyweshi mpaka wachungaji warudishe (wanyama wao), na baba yetu ni mzee sana.' Basi (Musa) akawanyweshea, kisha akarudi kivulini (akiwa amechoka) akasema, 'Mola wangu, bila shaka mimi ni muhitaji wa kheri yoyote utakayoniteremshia.'" [Qur'an, 28:23–24].

### Mazingatio

Sehemu hii ya simulizi ya Mtume Musa (amani ya Allah iwe juu yake) tunajifunza mambo kadhaa. Mosi, umuhimu wa tawakkul (kumtegemea Allah katika kila jambo). Shida yoyote inayomfika mja, anapaswa kuamini kuwa Allah ndiye mtatuzi wake.

Aidha, tunajifunza kuwa moja ya njia ya mja kusikilizwa dua zake na kutatuliwa shida zake ni kuwasaidia wenzake. Musa hakujali uchovu wa safari katika kuwasaidia wale mabinti, akiamini kuwa Allah hapotezi ujira wa watendao wema.

Funzo jingine ni haja ya kuwahurumia wanawake na kuwasaidia wanapokabiliana na kazi ngumu.

Katika toleo lijalo, tutaona jinsi Allah anavyomlipa mja wake (Musa) kwa tawakkul yake kubwa na wema huu aliowafanyia mabinti wale, in shaa Allah..

*Itaendelea inshaAllah*

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Je, mkate unaongeza uzito hata bila kula kalori nyingi zaidi? Utafiti waibua mjadala

Kwa muda mrefu, mjadala kuhusu kuongezeka kwa uzito umejikita katika kalori: kula zaidi, unanenepa; kula kidogo, unapungua. Lakini utafiti mpya unapendekeza kuwa picha inaweza kuwa tata zaidi. Inaonekana si kiasi cha chakula pekee kinachohusika—bali aina ya chakula na jinsi mwili unavyokichakata.




Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa na ScienceDaily, watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Osaka Metropolitan nchini Japan wamegundua kuwa vyakula vyenye wanga mwingi kama mkate, mchele na ngano vinaweza kusababisha kuongezeka kwa uzito—hata bila kuongeza kiasi cha kalori zinazoliwa.

Utafiti huu unaingia moja kwa moja katika mjadala mkubwa wa lishe: je, tatizo ni kula sana au ni aina ya chakula tunachokula?

Kwanza, watafiti walifanya majaribio kwa kutumia panya ili kuchunguza tabia ya ulaji na mabadiliko ya kimetaboli. Panya walipewa chaguo kati ya chakula chao cha kawaida na vyakula vyenye wanga mwingi kama unga wa ngano, mkate na mchele. Matokeo yalikuwa ya kushangaza: panya walipendelea vyakula vya wanga kwa kiwango kikubwa, wakiacha kabisa chakula chao cha kawaida.

Lakini jambo la kuvutia zaidi lilikuja baada ya hapo.

Pili, licha ya kwamba panya hawakuongeza sana kiwango cha kalori walizokula, waliongeza uzito na mafuta mwilini. Hii inaenda kinyume na dhana ya kawaida kwamba uzito huongezeka tu pale unapokula kalori nyingi zaidi. Badala yake, inaonyesha kuwa mwili unaweza kubadilika namna unavyotumia nishati kulingana na aina ya chakula.

Tatu, uchambuzi wa kina ulionyesha kuwa ongezeko hili la uzito halikutokana na kula kupita kiasi, bali kupungua kwa matumizi ya nishati mwilini. Kwa lugha rahisi, miili ya panya ilianza "kuchoma" kalori chache zaidi, hali iliyochangia kuongezeka kwa mafuta mwilini.

Hii inaibua hoja muhimu: huenda baadhi ya vyakula vinaathiri kasi ya kimetaboli (metabolism), na si tu kiasi cha nishati kinachoingia mwilini.

Nne, watafiti pia waligundua mabadiliko katika damu na ini la panya. Kulikuwa na ongezeko la asidi ya mafuta katika damu, pamoja na kupungua kwa baadhi ya amino asidi muhimu. Aidha, ini lilionyesha dalili za kuongezeka kwa utengenezaji wa mafuta. Hii inaonyesha kuwa vyakula vya wanga vinaweza kubadilisha mfumo mzima wa kimetaboli, si tu uzito wa mwili. Tano, jambo jingine la kuvutia ni kwamba panya waliokula mlo wenye mafuta mengi pamoja na unga wa ngano hawakuongezeka uzito kwa kiwango sawa na wale waliokula mlo wa mafuta pamoja na chakula cha kawaida. Hii inaonyesha kuwa tatizo si mafuta pekee kama ilivyoaminika kwa muda mrefu, bali ni mchanganyiko wa vyakula na namna vinavyoathiri mwili.

Hata hivyo, ni muhimu kuwa makini katika kutafsiri matokeo haya.

Utafiti huu ulifanywa kwa panya, si binadamu. Ingawa panya hutumika sana katika tafiti za kisayansi kwa sababu mifumo yao ya mwili inafanana kwa kiasi fulani na binadamu, si kila matokeo yanaweza kuhamishwa moja kwa moja kwa wanadamu.

Watafiti wenyewe wanakiri hili na wanasema hatua inayofuata ni kufanya tafiti kwa binadamu ili kuona kama matokeo haya yanafanana katika maisha halisi.

Hata hivyo, utafiti huu unaongeza mjadala muhimu katika lishe ya kisasa. Unatoa hoja kwamba si sahihi kuangalia kalori pekee bila kuzingatia ubora wa chakula. Vyakula tofauti vinaweza kuwa na athari tofauti kwa mwili, hata kama vina kiwango sawa cha kalori.

# Muabudu Mola wako mpaka yakufikie mauti

**Imepokewa hadith kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) kuwa siku moja Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimwambia Bilal wakati wa sala ya Alfajiri: "Ewe Bilal! Nisimulie kuhusu amali uliyoifanya katika Uislamu unayoitarajia zaidi (kupata thawabu zake), kwani nilisikia mkanyago wa viatu vyako mbele yangu huko Peponi."**
**Bilal (Allah amridhie) akajibu: "Sijawahi kufanya amali yoyote ninayoitarajia zaidi malipo yake kwa Allah, isipokuwa sijawahi kutia udhu wakati wowote wa usiku au mchana bila kusali kwa udhu huo kile nilichoandikiwa kusali."**
***[Bukhari na Muslim].***

## Mafundisho ya hadith

Makusudio ya sharia ya Allah kuhusu amali njema si tu kuzifanya, bali pia kuzidumisha. Kusitisha matendo mema au kuyaacha kwa sababu ya uvivu ni kinyume na mafundisho ya dini, ambayo inamtaka Muislamu kudumisha ibada. Qur'an Tukufu imenukuu maneno ya Nabii Isa (amani iwe juu yake) akisema: "...na ameniusia (Mola wangu) kusimamisha sala na kutoa zaka maadamu niko hai." [Qur'an, 19:31]. Pia Allah anasema: "Na muabudu Mola wako mpaka ikufikie yakini (mauti)." [Qur'an, 15:99].

Aya hizi zinafundisha kuwa Muislamu ana wajibu wa kutekeleza ibada hadi mwisho wa maisha yake, si kwa kipindi maalum tu. Miongoni mwa sifa za waja wema ni kudumu katika ibada, kama Allah anavyosema: "Hakika binadamu ameumbwa katika hali ya pupa; inapompata shari hulalamika, na inapompata kheri huwa bahili (kwa sababu ya uchoyo), isipokuwa wanaosali, ambao katika sala zao ni wenye kudumu." [Qur'an, 70:19–23].

Katika aya hizi, Allah Ta'ala anatupa ujumbe kuwa ibada na matendo mema yanapaswa kuwa ya kudumu na endelevu, si ya muda mfupi au ya vipindi vinavyokatika.

Kudumisha matendo mema ni miongoni mwa sababu kubwa za kupata mapenzi ya Allah Ta'ala, ambalo ndilo lengo kuu la waumini. Katika hadithil Qudsy, Mwenyezi Mungu anasema: "Yeyote anayemfanyia uadui walii wangu nimemtangazia vita. Na hajikurubishi kwangu mja wangu kwa kitu ninachokipenda zaidi kuliko yale niliyomfaradhishia. Na mja wangu ataendelea kujikurubisha kwangu kwa ibada za Sunna mpaka nampenda.

"Na nikimpenda, nitakuwa masikio yake anayosikia kwayo, macho yake anayotazama kwayo, mkono wake anaokamatia, na mguu wake anaotembelea. Na akiniomba nitampa, na akitaka hifadhi nitamlinda. Na sikusita katika jambo lolote kama ninavyosita katika kuichukua roho ya mja wangu muumini; yeye anachukia kufa na Mimi nachukia kumdhuru." [Bukhari].

Mja hupata mapenzi haya na ukaribu na Mola wake kwa kudumu katika ibada za faradhi na za Sunna, pamoja na kufanya mema mengine.

## Kupata mwisho mwema

Miongoni mwa sababu za kupata mwisho mwema ni kudumu katika matendo mema. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Allah anapomtakia kheri mja wake humtumia kabla ya kufa kwake." Masahaba wakauliza: "Ewe Mtume wa Allah, vipi humtumia?" Akasema: "Humuwezesha kufanya amali njema kisha humfisha akiwa juu ya amali hiyo." [Tirmidhi].

Katika riwaya nyingine Mtume amesema, Allah anapomtakia mja wake kheri humfungulia milango ya kufanya kheri kabla ya kufa kwake, kisha humchukua akiwa katika hali hiyo, [Sahih Al–Jaami'u].

## Thawabu bila kutenda

Kudumu katika ibada huleta utulivu na kuondoa majuto wakati wa ugonjwa au udhaifu. Mtu aliyekuwa na mazoea ya kufanya ibada, kisha akashindwa kutokana na ugonjwa au safari, huendelea kuandikiwa thawabu kama zile alizokuwa akizipata alipokuwa mzima au kwenye mji wake.

## Jinsi ya kudumu katika ibada

Miongoni mwa njia za kudumu katika ibada ni kuzifanya kwa kiasi (wastani). Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Fanyeni ibada mnazoweza, kwani Allah hachoki mpaka nyinyi mchoke." [Muslim]. Hadith hii inaonesha kuwa ibada chache lakini za kudumu ni bora kuliko nyingi zinazokatika.

Aidha, Muislamu anapaswa kuomba msaada kwa Allah bila kuchoka. Mtume amesema: "Usiache kusema baada ya kila sala: 'Allahumma a'inni 'ala dhikrika washukrika wahusni 'ibadatika.'" Maana yake: "Ewe Allah, nisaidie kukukumbuka, kukushukuru na kukuabudu vizuri." [Tirmidhi].

Pia Mtume alikuwa akisema mara kwa mara: "Ewe mgeuzaji wa nyoyo, thibitisha moyo wangu juu ya dini yako." [Tirmidhi].

Kulainisha moyo ni sababu nyingine ya kudumu katika ibada. Mtume amesema: "Katika mwili kuna kipande cha nyama; kikitengemaa mwili wote hutengemaa, na kikiharibika mwili wote huharibika, nacho ni moyo."

Muislamu anaweza kulainisha moyo wake kwa kuongeza matendo mema, kushukuru, kumcha Allah, kufanya ibada kwa ikhlas, na kujiepusha na maasi, kiburi, husuda na ria. Madhambi haya yanaweza kumzuia mtu kufanya mema.

Katika kufafanua hilo, Imam Ibnu Qayyim (Allah amrehemu) amesema: "Dhambi moja inaweza kukuzuia kufanya ibada nyingi nzuri..." Aidha, kushirikiana na marafiki wema ni sababu muhimu ya kudumu katika ibada, kwani mtu huathiriwa na tabia za watu wanaomzunguka.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Aina nne za malezi ya watoto: ipi bora?



Wazazi wengi hujiuliza swali moja muhimu: ni aina gani ya malezi inayofaa kwa mtoto wangu? Ukweli ni kwamba hakuna "mwongozo rasmi" wa kulea watoto. Hata hivyo, saikolojia ya maendeleo imejaribu kutoa mwanga kupitia dhana ya aina nne za malezi—zilizoanzishwa na mwanasaikolojia Diana Baumrind katika miaka ya 1960. Kwa mujibu wa tafiti, aina hizi za malezi zinatofautishwa na mambo mawili makuu: upendo na uelewa (responsiveness) na nidhamu au udhibiti (demandingness). Mchanganyiko wa vipengele hivi huunda mitindo minne tofauti ya malezi, kila mmoja ukiwa na athari zake kwa mtoto.

## Mosi: Malezi ya usawa (authoritative): upendo + mipaka

Hii ndiyo aina inayopendekezwa zaidi na wataalamu. Mzazi anaweka sheria na mipaka, lakini pia anaonyesha upendo, kusikiliza na kuelewa mtoto. Hapa, mawasiliano ni ya pande mbili—mtoto anaweza kuuliza, kueleza hisia na kushiriki katika maamuzi. Katika mtindo huu, nidhamu hutumika kufundisha, si kuadhibu. Mtoto anajifunza kujidhibiti, kufikiri na kutatua matatizo. Tafiti zinaonyesha kuwa watoto wanaolelewa kwa mtindo huu huwa na kujiamini zaidi, uwezo mzuri wa kijamii na mafanikio ya kitaaluma. Kwa lugha rahisi, katika aina hii ya malezi kuna uwiano wa upendo na nidhamu.

## Pili: Malezi ya ukali (authoritarian): nidhamu kali bila uelewa

Hapa mzazi anaweka sheria kali na anatarajia utii bila mjadala. Kauli kama "kwa sababu nimesema mimi" ni za kawaida katika mtindo huu.

Tatizo ni kwamba, ingawa watoto wanaweza kuwa watiifu kwa muda mfupi, mara nyingi hukosa uwezo wa kujitegemea na kujiamini. Tafiti zinaonyesha kuwa malezi haya yanaweza kuhusishwa na matatizo ya kisaikolojia na tabia baadaye maishani.

Kwa kifupi katika aina hii ya malezi, kuna udhibiti mwingi, lakini upendo na mawasiliano ni mdogo.

## Tatu: Malezi ya kulegeza (permissive): upendo bila mipaka

Katika mtindo huu, mzazi ni mpole sana na mara nyingi huacha mtoto kufanya anavyotaka. Kuna upendo mwingi, lakini hakuna nidhamu ya kutosha.

Mzazi anaweza kuwa kama rafiki zaidi kuliko mlezi. Ingawa watoto wanahisi kupendwa, ukosefu wa mipaka unaweza kusababisha matatizo kama ukosefu wa nidhamu binafsi, tabia zisizo thabiti au utegemezi kupita kiasi.

Kwa lugha nyingine katika aina hii ya malezi kuna upendo mwingi, lakini pia hakuna mwongozo.

## Nne: Malezi ya kupuuza (uninvolved): hakuna upendo wala mwongozo

Hii ndiyo aina hatari zaidi. Mzazi hana ushiriki wa karibu katika maisha ya mtoto—wala kihisia wala kimaadili. Anaweza kutoa mahitaji ya msingi kama chakula au makazi, lakini anakosa uwepo wa kihisia.

Watoto wanaokulia katika mazingira haya mara nyingi hukumbwa na changamoto kubwa: upweke, matatizo ya kitabia na hata matatizo ya akili wanapokua. Kwa kifupi aina hii ya malezi, hakuna uhusiano wa kweli kati ya mzazi na mtoto.

## Je, mzazi anapaswa kuchagua mtindo mmoja tu?

Hapa ndipo mjadala unakuwa wa kuvutia. Wataalamu wanasema wazazi wengi hawakai kwenye kundi moja tu. Badala yake, hutumia mitindo tofauti kulingana na mazingira. Kwa mfano, katika hali ya hatari, mzazi anaweza kuwa mkali zaidi. Lakini katika hali ya kawaida, anaweza kuwa mpole na msikivu.

Hata hivyo, ujumbe mkuu wa tafiti ni huu: mtoto hukua vizuri zaidi pale anapopata upendo pamoja na mipaka iliyo wazi.Hii ndiyo sababu malezi ya usawa (authoritative) yanaonekana kuwa bora zaidi—kwa sababu yanachanganya vipengele vyote viwili.

Aina ya malezi si tu mtindo wa kulea—ni msingi wa maisha ya mtoto ya baadaye. Inaathiri jinsi anavyojiona, jinsi anavyohusiana na wengine na jinsi anavyokabiliana na changamoto.

Kwa mzazi, swali muhimu si "ni mkali kiasi gani?" au "ni mpole kiasi gani?" bali ni:

"Je, ninaweza kuwa na upendo na mipaka kwa wakati mmoja?" Kwa sababu mwishowe, watoto hawahitaji wazazi wakali kupita kiasi wala wapole kupita kiasi—wanahitaji wazazi wanaowaongoza kwa upendo, hekima na usawa.

UKHTI FATIMA SS

# Je, lafudhi yako inaathiri jinsi ujumbe wako unavyopokelewa?

Katika dunia ya leo yenye mawasiliano ya kimataifa, watu wengi hulazimika kuzungumza lugha ambazo si zao za kwanza. Hali hii huleta swali la kawaida lakini nyeti: je, lafudhi (accent) inaweza kuathiri namna watu wanavyokusikiliza au kukuchukulia? Utafiti wa hivi karibuni unaonyesha jibu si rahisi—lakini kwa kiasi fulani ni "ndiyo."

Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa kwenye Psychology Today, watafiti waligundua kuwa wazungumzaji wenye lafudhi isiyo ya asili (non-native accent) hupata usikivu mdogo ukilinganishwa na wale wenye lafudhi ya asili ya lugha. Hii ina maana kwamba tatizo si tu ujumbe unaotolewa, bali pia namna unavyotolewa.

Utafiti huo ulitumia maelfu ya hotuba kutoka jukwaa la TED Talks kuchunguza jinsi watazamaji wanavyoshiriki (engagement). Matokeo yalionyesha kuwa hotuba zilizotolewa kwa lafudhi ya asili zilipata "likes" na maoni mengi zaidi kuliko zile zenye lafudhi ya kigeni—hata pale mada ilikuwa sawa. Hii inaibua swali kubwa: je, watu wanahukumu ujumbe au mtoa ujumbe?

Watafiti wanatoa sababu mbili kuu zinazoeleza hali hii. Sababu ya kwanza ni mitazamo ya kijamii (stereotypes). Lafudhi mara nyingi huhusishwa na asili ya mtu—nchi, elimu au hata uwezo wake. Hivyo, bila kujua, wasikilizaji wanaweza kumchukulia mtu mwenye lafudhi ya kigeni kuwa hana ujuzi au hana uhakika, hata kama si kweli.

Sababu ya pili ni kile kinachoitwa urahisi wa kuelewa (processing fluency). Kwa lugha rahisi, watu hupenda kusikiliza kile kinachoeleweka kwa urahisi. Lafudhi ya kigeni inaweza kuhitaji juhudi zaidi ya akili ili kufuatilia maneno, hivyo baadhi ya wasikilizaji hupoteza umakini mapema. Hii si lazima iwe kwa makusudi—ni jinsi ubongo unavyofanya kazi.

Lakini hapa ndipo mjadala unakuwa wa kuvutia zaidi. Je, hii ina maana kwamba watu wenye lafudhi tofauti wanapaswa kubadilika ili wakubalike? Si lazima.

Kwa kweli, watafiti wanasisitiza kuwa tatizo si lafudhi yenyewe, bali ni mtazamo wa jamii. Wanasema accentism—yaani ubaguzi unaotokana na lafudhi—ni aina ya ubaguzi ambayo haijajadiliwa sana ukilinganisha na ubaguzi wa rangi au jinsia. Hii ina maana kwamba suluhisho halipaswi kuwa kubadilisha watu, bali kubadilisha namna tunavyowasikiliza.

Hata hivyo, kwa upande wa mawasiliano ya vitendo, kuna mikakati inayoweza kusaidia. Kwa mfano, matumizi ya manukuu (subtitles), tafsiri ya papo kwa papo au teknolojia za AI zinazosaidia kusawazisha sauti zinaweza kupunguza ugumu wa kuelewa. Pia, majukwaa ya kidijitali yanaweza kusaidia kwa kutoa nafasi sawa kwa wazungumzaji wote bila kujali lafudhi zao.

Kwa wazungumzaji wenyewe, kuna masomo muhimu hapa. Kwanza, lafudhi si kizuizi kamili—ni changamoto inayoweza kudhibitiwa. Pili, uwazi wa ujumbe ni muhimu zaidi kuliko ukamilifu wa matamshi. Utafiti unaonyesha kuwa hata kama lafudhi inaathiri mtazamo wa awali, ubora wa hoja bado una nafasi ya kushinda.

Kwa upande mwingine, wasikilizaji pia wana jukumu. Katika dunia inayozidi kuwa ya kimataifa, uwezo wa kusikiliza lafudhi tofauti ni ujuzi muhimu. Ni sehemu ya kuheshimu utofauti na kuhakikisha kuwa maarifa hayasahauliki kwa sababu ya namna yanavyotolewa.

Kwa kumalizia, niseme kuwa lafudhi inaweza kuathiri jinsi ujumbe unavyopokelewa, lakini haipaswi kuamua thamani ya ujumbe huo. Katika mawasiliano ya kisasa, changamoto si tu kuzungumza, bali kusikiliza kwa haki. Kadri tunavyoongeza ufahamu kuhusu accentism, ndivyo tunavyofungua milango kwa sauti nyingi zaidi kusikika.

Mwisho wa siku, kila mtu ana lafudhi. Tofauti ni kwamba baadhi zinaonekana kuwa "za kawaida" kuliko nyingine. Lakini ukweli ni kwamba, katika dunia ya leo, utofauti huo ndiyo nguvu—sio udhaifu.

Afya
Pure Drinking water

"Afya" is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com





NA UKHTI FATIMA

# Mbinu za kuepuka riba katika maisha ya kisasa

**Katika Uislamu, riba si tu kosa la kifedha bali ni ukiukwaji wa maadili ya haki na usawa. Qur'an inaweka wazi msimamo huu: "Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharamisha riba." [Qur'an, 2:275].**

**Marufuku hii inalenga kulinda jamii dhidi ya unyonyaji na kuzuia mifumo inayozalisha pengo kubwa la kiuchumi. Hata hivyo, katika ulimwengu wa leo unaotegemea mifumo ya riba, swali la msingi linabaki: Muislamu anawezaje kuishi bila riba?**

**Kwanza, ni muhimu kuelewa riba kwa kina. Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, riba inajumuisha ongezeko lisilo la haki katika mikopo (riba al-nasi'ah) na ubadilishanaji usio sawa wa bidhaa (riba al-fadl). Uelewa huu humsaidia mtu kutambua riba hata inapojificha katika mikataba ya kisasa ya kifedha.**

**Changamoto kubwa ni kwamba mifumo ya kifedha duniani imejengwa juu ya riba kiasi kwamba hata shughuli za kawaida kama kununua nyumba, kutumia kadi za mkopo au kuweka akiba benki mara nyingi huhusisha riba kwa namna fulani. Hivyo, kuepuka riba kunahitaji mkakati wa makusudi, si maamuzi ya bahati nasibu.**

## Mbinu za vitendo za kuepuka riba

Kwanza ni kuishi bila madeni inapowezekana. Nidhamu ya kifedha—kupanga matumizi, kuishi ndani ya uwezo na kuepuka mikopo isiyo ya lazima—ni msingi wa maisha yasiyo na riba. Matumizi ya kadi za mkopo yanapaswa kudhibitiwa kwa kulipa deni lote kabla ya muda wa riba kuanza, au kuepukwa kabisa ikiwa haiwezekani kudhibiti matumizi.

Pili, ni kuchagua mifumo ya kifedha inayokubalika Kiislamu. Badala ya mikopo ya riba, taasisi za Kiislamu hutumia mifumo ya ushirikiano kama musharaka (ubia) au murabaha (uuzaji kwa faida inayojulikana). Kwa mfano, katika ununuzi wa nyumba, mfumo wa umiliki wa pamoja huruhusu mnunuzi kumiliki mali hatua kwa hatua bila riba. Hii inaonyesha kuwa mbadala wa riba upo, ingawa unahitaji utafutaji na uelewa.

Tatu, ni kuwekeza na kuweka akiba kwa njia halali. Badala ya akaunti zinazozalisha riba, mtu anaweza kuchagua akaunti zisizo na riba au uwekezaji unaofuata misingi ya Sharia, kama biashara halali au mali zisizohusisha haramu. Aidha, baadhi ya watu huchagua kutoa riba yoyote wanayopokea bila kukusudia kama sadaka ili kujitakasa nayo.

Nne, ni kuwa makini katika mikataba ya biashara. Riba mara nyingi hujificha katika masharti madogo ya mikataba. Ndiyo maana wataalamu wanashauri kushauriana na wanazuoni au wataalamu wa fedha za Kiislamu kabla ya kuingia mikataba mikubwa.

Tano, ni kutumia mbinu za kijamii za kifedha. Jamii inapendekeza njia kama kukopa kutoka kwa familia au marafiki, au kutumia qard hasan—mkopo mwema usio na riba unaotolewa kwa nia ya kusaidia. Hii huimarisha mshikamano wa kijamii na kupunguza utegemezi wa taasisi za riba.

Sita, ni kupanga manunuzi makubwa kwa njia mbadala. Badala ya kununua kwa mkopo wa riba, mtu anaweza kuchagua kukodisha au kuweka akiba hadi aweze kununua kwa fedha taslimu. Njia hii, ingawa ni ya polepole, huondoa mzigo wa madeni ya muda mrefu.

Saba, ni kujielimisha mara kwa mara. Maarifa ya fedha za Kiislamu yanabadilika kadri mifumo mipya inavyoibuka. Kujifunza kupitia wanazuoni na wataalamu husaidia kufanya maamuzi sahihi na kuepuka mitego ya kisasa ya kifedha.

Nane, ni kujenga mtazamo wa kuridhika (qana'ah) na kumtegemea Mwenyezi Mungu (tawakkul). Maisha yasiyo na riba yanahitaji mtu kukubali mipaka ya kipato chake na kuepuka shinikizo la kijamii la kuishi juu ya uwezo wake. Qur'an inahimiza: "Na anayemcha Mwenyezi Mungu, Atamfanyia njia ya kutokea." [Qur'an, 65:2–3]

Kwa ujumla, kuepuka riba katika dunia ya leo si jambo rahisi, lakini linawezekana. Linahitaji mchanganyiko wa elimu, nidhamu na imani. Kwa kuunganisha mbinu za kifedha zilizo halali, maamuzi ya busara ya matumizi na utegemezi kwa Mwenyezi Mungu, Muislamu anaweza kujenga maisha yenye usawa, haki na baraka. Mwishowe, mapambano dhidi ya riba si tu ya kiuchumi—ni juhudi ya kulinda utu na maadili ya jamii nzima.

